القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

Juzuu - FOUR (Lan Tanalu)

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy

83. Je! Wanataka dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kinamtii Yeye, kikipenda kisipende? Na Kwake watarejeshwa wote.

أَفَغَيْرَ دِينِ اللَّهِ يَبْغُونَ وَلَهُ أَسْلَمَ مَن فِي السَّمَٰوَٰتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿٨٣﴾

84. Sema: "Tumemwamini Mwenyezi Mungu, na yale tuliyoteremshiwa na aliyoteremshiwa Ibrahimu na Ismaili na Ishaka na Yakubu na watoto (wake), na yale aliyopewa Musa na Isa na Manabii (wengine) kutoka kwa Mola wao. Hatubagui baina yao hata mmoja, na sisi tunanyenyekea Kwake.

قُلْ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ عَلَيْنَا وَمَا أُنزِلَ عَلَىٰ إِبْرَٰهِيمَ وَإِسْمَٰعِيلَ وَإِسْحَٰقَ وَيَعْقُوبَ وَالْأَسْبَاطِ وَمَا أُوتِيَ مُوسَىٰ وَعِيسَىٰ وَالنَّبِيُّونَ مِن رَّبِّهِمْ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِّنْهُمْ وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ ﴿٨٤﴾

85. Na anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye khasara (kubwa kabisa).

وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَٰمِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْءَاخِرَةِ مِنَ الْخَٰسِرِينَ ﴿٨٥﴾

86. Mwenyezi Mungu atawaongozaje (kwendea haki) watu waliokufuru baada ya kuamini kwao, na wakashuhudia ya kwamba Mtume (huyu) ni wa haki, na zikawafikia hoja zilizo wazi? Mwenyezi Mungu hawaongozi watu madhalimu.

كَيْفَ يَهْدِي اللَّهُ قَوْمًا كَفَرُوا بَعْدَ إِيمَٰنِهِمْ وَشَهِدُوا أَنَّ الرَّسُولَ حَقٌّ وَجَاءَهُمُ الْبَيِّنَٰتُ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّٰلِمِينَ ﴿٨٦﴾

87. Hao malipo yao ni kuwa iko juu yao laana ya Mwenyezi Mungu, na ya Malaika na ya watu wote

أُولَٰئِكَ جَزَاؤُهُمْ أَنَّ عَلَيْهِمْ لَعْنَةَ اللَّهِ وَالْمَلَٰئِكَةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿٨٧﴾

88. Humo watakaa milele. Hawatapunguziwa adhabu wala hawatapewa nafasi (ya kupumzika)

خَٰلِدِينَ فِيهَا لَا يُخَفَّفُ عَنْهُمُ الْعَذَابُ وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿٨٨﴾

89. Isipokuwa wale waliotubu baada ya hayo na wakatengeneza (amali zao). (Hao Mungu atawasamehe) kwani Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا مِن بَعْدِ ذَٰلِكَ وَأَصْلَحُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٨٩﴾

90. Hakika wale waliokufuru baada ya kuamini kwao, kisha wakazidi kukufuru; toba yao haitakubaliwa (kamwe), na hao ndio waliopotea (kweli kweli).

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بَعْدَ إِيمَٰنِهِمْ ثُمَّ ازْدَادُوا كُفْرًا لَّن تُقْبَلَ تَوْبَتُهُمْ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الضَّالُّونَ ﴿٩٠﴾

91. Hakika wale waliokufuru, na wakafa hali ni makafiri, basi haitakubaliwa kwa mmoja wao ijapokuwa katoa fidia ya dhahabu kwa kuijaza ardhi yote. Hao ndio watakaopata adhabu iumizayo, wala hawatakuwa na wasaidizi.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَمَاتُوا وَهُمْ كُفَّارٌ فَلَن يُقْبَلَ مِنْ أَحَدِهِم مِّلْءُ الْأَرْضِ ذَهَبًا وَلَوِ افْتَدَىٰ بِهِ أُولَٰئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ وَمَا لَهُم مِّن نَّٰصِرِينَ ﴿٩١﴾

92. Hamtaweza kuufikia wema (khasa) mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda; na cho chote mnachokitoa, basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua.

لَن تَنَالُوا الْبِرَّ حَتَّىٰ تُنفِقُوا مِمَّا تُحِبُّونَ وَمَا تُنفِقُوا مِن شَيْءٍ فَإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ ﴿٩٢﴾

---

84. Hii ndiyo itikadi ya Uislamu kama tulivyobainisha katika maelezo ya Aya ya mwisho ya *Suratil Baqarah.*

92. Cho chote cha kheri anachokitoa mtu katika njia za kheri anapata thawabu. Lakini kila anapotoa anachokipenda zaidi ndio bora. Ukimpa masikini nguo usiyoitaka utapata thawabu. Lakini ukimpa unayoitaka utapata thawabu zaidi.

93. Kila chakula kilikuwa halali kwa kizazi cha Israili (Mayahudi) isipokuwa kile alichojiharimishia Israili mwenyewe — kabla haijateremshwa Taurati. Sema: "Leteni hiyo Taurati muisome ikiwa mnasema kweli."

كُلُّ ٱلطَّعَامِ كَانَ حِلًّا لِّبَنِيٓ إِسۡرَٰٓءِيلَ إِلَّا مَا
حَرَّمَ إِسۡرَٰٓءِيلُ عَلَىٰ نَفۡسِهِۦ مِن قَبۡلِ أَن تُنَزَّلَ
ٱلتَّوۡرَىٰةُۚ قُلۡ فَأۡتُواْ بِٱلتَّوۡرَىٰةِ فَٱتۡلُوهَآ إِن كُنتُمۡ
صَٰدِقِينَ ٩٣

94. Na wo wote watakaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu baada ya haya, basi hao ndio madhalimu (wa nafsi zao).

فَمَنِ ٱفۡتَرَىٰ عَلَى ٱللَّهِ ٱلۡكَذِبَ مِنۢ بَعۡدِ ذَٰلِكَ
فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلظَّٰلِمُونَ ٩٤

95. Sema: "Mwenyezi Mungu amesema kweli." Basi fuateni mila ya Ibrahimu aliyekhalisika (na nyendo za upotofu), wala hakuwa miongoni mwa washirikina.

قُلۡ صَدَقَ ٱللَّهُۗ فَٱتَّبِعُواْ مِلَّةَ إِبۡرَٰهِيمَ
حَنِيفٗاۖ وَمَا كَانَ مِنَ ٱلۡمُشۡرِكِينَ ٩٥

96. Kwa yakini Nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu (kufanya ibada) ni ile iliyoko Makka, yenye baraka na uwongozi kwa ajili ya walimwengu wote.

إِنَّ أَوَّلَ بَيۡتٖ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبَارَكٗا
وَهُدٗى لِّلۡعَٰلَمِينَ ٩٦

97. Humo mna Ishara zilizo wazi (za kuonyesha utukufu wake na ukongwe wake. Miongoni mwa hizo ni) mahali alipokuwa akisimama Ibrahimu, na anayeingia (nchi hiyo) anakuwa katika salama. Na Mwenyezi Mungu amewawajibishia watu wafanye Hija katika Nyumba hiyo; yule awezaye kufunga safari kwenda huko. Na atakayekanusha (asende, na hali ya kuwa anaweza) basi Mwenyezi Mungu si mhitaji kuwahitajia walimwengu.

فِيهِ ءَايَٰتُۢ بَيِّنَٰتٞ مَّقَامُ إِبۡرَٰهِيمَۖ وَمَن دَخَلَهُۥ
كَانَ ءَامِنٗاۗ وَلِلَّهِ عَلَى ٱلنَّاسِ حِجُّ ٱلۡبَيۡتِ مَنِ
ٱسۡتَطَاعَ إِلَيۡهِ سَبِيلٗاۚ وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَنِيٌّ
عَنِ ٱلۡعَٰلَمِينَ ٩٧

98. Sema: "Enyi watu mliopewa Kitabu! Kwa nini mnazikataa hoja za Mwenyezi Mungu, hali Mwenyezi Mungu ni shahidi juu ya yote mnayoyatenda?

قُلۡ يَٰٓأَهۡلَ ٱلۡكِتَٰبِ لِمَ تَكۡفُرُونَ بِـَٔايَٰتِ ٱللَّهِ
وَٱللَّهُ شَهِيدٌ عَلَىٰ مَا تَعۡمَلُونَ ٩٨

99. Sema: "Enyi mliopewa Kitabu! Kwa nini mnawazuilia (watu) na njia (dini) ya Mwenyezi Mungu; wale walioamini? Mkaitafutia kosa, na hali mnashuhudia (kuwa ni njia ya Mwenyezi Mungu isiyokuwa na kosa). Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na mnayoyatenda."

قُلۡ يَٰٓأَهۡلَ ٱلۡكِتَٰبِ لِمَ تَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ
ٱللَّهِ مَنۡ ءَامَنَ تَبۡغُونَهَا عِوَجٗا وَأَنتُمۡ
شُهَدَآءُۗ وَمَا ٱللَّهُ بِغَٰفِلٍ عَمَّا تَعۡمَلُونَ ٩٩

100. Enyi mlioamini! Mkiwatii baadhi ya wale waliopewa Kitabu, watakurudisheni kuwa makafiri baada ya Uislamu wenu.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِن تُطِيعُواْ فَرِيقٗا مِّنَ
ٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلۡكِتَٰبَ يَرُدُّوكُم بَعۡدَ إِيمَٰنِكُمۡ
كَٰفِرِينَ ١٠٠

101. Na mnakanushaje, hali nyinyi mnasomewa Aya za Mwenyezi Mungu, na Mtume wake yuko

وَكَيۡفَ تَكۡفُرُونَ وَأَنتُمۡ تُتۡلَىٰ عَلَيۡكُمۡ ءَايَٰتُ

93. Mayahudi walimwambia Mtume "Wewe hufuati mwendo wa Nabii Ibrahimu ingawa unajidai unafuata. Mbona unakula nyama ya ngamia; na Nabii Ibrahimu hakuwa akila nyama ya ngamia?" Ndiyo wanasutwa hapa kuwa: Ni uwongo huo; na dalili ni hiyo Taurati. Nawaifungue hiyo Taurati wataona kuwa Nabii Yaaqubu (Israili) — si Nabii Ibrahimu — ndiye aliyejiharimishia kula nyama ya ngamia mwenyewe kwa nafsi yake bila ya kulazimishwa na Mwenyezi Mungu.

96. Hapa inabainishwa kuwa nyumba ya mwanzo iliyowekewa watu kufanya Ibada ni Al Kaaba, si Baytil Muqaddas, kama walivyokuwa wakidai Mayahudi. Na alama ya haya ni hizo dalili zilizotajwa.

pamoja na nyiye? Na mwenye kumshika Mwenyezi Mungu sawasawa, basi yeye amekwishaongozwa katika njia iliyonyoka.

اللَّهِ وَفِيكُمْ رَسُولُهُ ۗ وَمَن يَعْتَصِم بِاللَّهِ فَقَدْ
هُدِيَ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿١٠١﴾

102. Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife isipokuwa mmekwishakuwa Waislamu kamili.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلَا
تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ ﴿١٠٢﴾

103. Na shikamaneni kwa kamba (dini) ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu. (Zamani) mlikuwa maadui; naye akaziunganisha nyoyo zenu; hivyo, kwa neema yake, mkawa ndugu. Na mlikuwa ukingoni mwa shimo la Moto (wa Jahannam), naye akakuokoeni nalo. Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubainishieni Aya zake ili mpate kuongoka.

وَاعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا ۚ
وَاذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنتُمْ أَعْدَاءً
فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُم بِنِعْمَتِهِ إِخْوَانًا
وَكُنتُمْ عَلَىٰ شَفَا حُفْرَةٍ مِّنَ النَّارِ فَأَنقَذَكُم
مِّنْهَا ۗ كَذَٰلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ
تَهْتَدُونَ ﴿١٠٣﴾

104. Na wawepo katika nyinyi watu wanaolingania kheri (Uislamu) na wanaoamrisha mema na wakakataza maovu. Na hao ndio watakaotengenekewa.

وَلْتَكُن مِّنكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ
وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ ۚ
وَأُولَٰئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٤﴾

105. Wala msiwe kama wale waliofarikiana na kukhitalifiana baada ya kuwafikia dalili zilizo wazi (za kuwakataza hayo). Na hao ndio watakaokuwa na adhabu kubwa

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ تَفَرَّقُوا وَاخْتَلَفُوا مِن بَعْدِ
مَا جَاءَهُمُ الْبَيِّنَاتُ ۚ وَأُولَٰئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ
عَظِيمٌ ﴿١٠٥﴾

106. (Katika) siku ambayo nyuso (nyingine) zitakuwa nyeupe, na nyuso (nyengine) zitakuwa nyeusi. Ama hao ambao nyuso zao zitakuwa nyeusi (wataambiwa): "Je! Mlikufuru baada ya imani yenu? Basi onjeni (uchungu wa) adhabu kwa kule kukanusha kwenu."

يَوْمَ تَبْيَضُّ وُجُوهٌ وَتَسْوَدُّ وُجُوهٌ ۚ فَأَمَّا
الَّذِينَ اسْوَدَّتْ وُجُوهُهُمْ أَكَفَرْتُم بَعْدَ
إِيمَانِكُمْ فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿١٠٦﴾

107. Ama hao ambao nyuso zao zitakuwa nyeupe, watakuwa katika rehema ya Mwenyezi Mungu. Wao humo watakaa milele.

وَأَمَّا الَّذِينَ ابْيَضَّتْ وُجُوهُهُمْ فَفِي
رَحْمَةِ اللَّهِ ۖ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿١٠٧﴾

---

102. Hapa inahimizwa kila wakati mtu awe juu ya Uislamu wake kamili — kwa kujiepusha na kila lililokatazwa na kufanya kila analoliweza — kwani hajui mtu mauti yatamjia wakati gani.

103. Hapa na katika Aya zifuatazo wanaambiwa Waislamu washikamane wote pamoja kwa jina la dini yao ya Uislamu. Wasifarikiane kwa jina la miji au kabila au vyama au mengineyo kama ilivyo sasa. Kufanya hivyo ni jukumu kubwa kabisa. Natuache upesi au khatari itakuwa kubwa kabisa na dhambi kubwa.

Watu wengine katika Aya waliyoita ya 104 wamepachikia maneno haya "Kamba ya Mungu ambayo Waislamu wakiishika watakaa katika hali ya umoja ni (1) Kurani; (2) Mjumbe wa Mungu; (3) Makhalifa wa Mjumbe wa Mungu. Katika Aya hii wanaonywa Waislamu wasifarikiane maana kufarikiana ni jambo la hatari sana kwao." Hiyo No. (2) na (3) wamemkusudia mtu wao na Makhalifa wake ambaye huyu aliyoko sasa ni wa tatu. Huu ukafiri wao wameupachika hapa, na kuwataka Waislamu wasiwapige vita — wawe pamoja nao, wasifarikiane nao. Wakajidai kuwa Mwenyezi Mungu kasema hivi. Hakutwambia sisi Mwenyezi Mungu kuwa tusiwakhalifu wanaokhalifu Uislamu. Tumeambiwa tuwakhalifu kweli kweli na kuwapiga vita vikali wanafiki hao. Tazama Aya ya 74 ya *Suratut Tawba* na Aya ya 9 ya *Suratut Tahrim* na nyinginezo. Basi sharti tumpige vita barabara mjumbe wao huyo waliojiwekea wenyewe na makhalifa wao waliojiwekea wenyewe huko Bara Hindi — Kadiyan kwao.

106. Yanatajwa madhila yatakayowapata wale wanaokhitalifiana kwa ajili ya yale yaliyokatazwa. Yatakuwa tu siku hiyo.

108. Hizi ni Aya za Mwenyezi Mungu tunakusomea kwa haki. Na Mwenyezi Mungu hataki kuwadhulumu walimwengu.

تلك ايت الله نتلوها عليك بالحق وما
الله يريد ظلما للعلمين ﴿١٠٨﴾

109. Na kila kilichomo mbinguni na kilichomo ardhini ni cha Mwenyezi Mungu; na mambo (yote) yatarejeshwa kwa Mwenyezi Mungu.

ولله ما في السموت وما في الارض والى الله
ترجع الامور ﴿١٠٩﴾

110. Nyinyi ndio umma bora kuliko umma zote zilizodhihirishiwa watu (ulimwenguni) — mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza yaliyo maovu, na mnamwamini Mwenyezi Mungu. Na kama wale waliopewa Kitabu wangaliamini (kama walivyoamrishwa) ingalikuwa bora kwao. (Lakini) miongoni mwao wako wanaoamini; na wengi wao wanatoka katika taa ya Mwenyezi Mungu.

كنتم خير امة اخرجت للناس تامرون
بالمعروف وتنهون عن المنكر وتؤمنون بالله
ولو امن اهل الكتب لكان خيرا لهم
منهم المؤمنون واكثرهم الفسقون ﴿١١٠﴾

111. Hawatakudhuruni (hao maadui zenu; khasa Mayahudi) ila udhia (mdogo tu hivi). Na kama watapigana nanyi basi watakupeni migongo (wakimbie); kisha hawatanusuriwa.

لن يضروكم الا اذى وان يقاتلوكم يولوكم
الادبار ثم لا ينصرون ﴿١١١﴾

112. Wamepigwa chapa ya dhila mahala po pote wanapokuwako; ila (kwa kushika) kamba (dini) ya Mwenyezi Mungu au kamba ya watu (wawasaidie; lakini wenyewe peke yao hawajitoshelezi). Na wamestahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu; na chapa ya dhila imepigwa juu yao. Haya ni kwa sababu ya wao kutoamini maneno ya Mwenyezi Mungu na kuwaua Manabii bila ya haki; haya ni kwa sababu waliasi na walikuwa wakiruka mipaka (aliyoiweka Mwenyezi Mungu).

ضربت عليهم الذلة اين ما ثقفوا الا
بحبل من الله وحبل من الناس وباءو
بغضب من الله وضربت عليهم المسكنة
ذلك بانهم كانوا يكفرون بايت الله
ويقتلون الانبياء بغير حق ذلك بما
عصوا وكانوا يعتدون ﴿١١٢﴾

113. Wao (waliopewa Kitabu) si wote sawa. Katika (hao) waliopewa Kitabu wamo watu waliotengenea — wanasoma Aya za Mwenyezi Mungu nyakati za usiku, na pia wanasujudu (yaani wamesilimu).

ليسوا سواء من اهل الكتب امة قائمة
يتلون ايت الله اناء اليل وهم يسجدون ﴿١١٣﴾

114. Wanamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na wanaamrisha mema na wanakataza maovu na wanayaendea mbio mambo mema. Na hao ndio miongoni mwa hao watendao mema (kweli kweli).

يؤمنون بالله واليوم الاخر ويامرون
بالمعروف وينهون عن المنكر
ويسارعون في الخيرت واولئك من
الصلحين ﴿١١٤﴾

115. Na kheri yo yote watakayoifanya hawatakanushiwa (thawabu zake). Na Mwenyezi Mungu anawajua wanaomcha (wakajiepusha na makatazo yake na wakafanya maamrisho yake).

وما يفعلوا من خير فلن يكفروه والله
عليم بالمتقين ﴿١١٥﴾

---

110. Hapa inatajwa sababu ya kuwa bora umma huu. Basi natushikamane nayo au hatutakuwa hivyo. Tazama Aya 143 ya *Suratul Baqarah*.

115. Hapa inabainishwa kuwa yo yote yule anayefanya mema kwa (a) Nia nzuri na (b) Kufuata alivyosema Mungu atalipwa tu mema yake.

116. Hakika wale waliokufuru hazitawafaa mali zao wala watoto wao hata kidogo mbele ya Mwenyezi Mungu; na hao ndio watu wa Motoni; watakaa humo milele.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَن تُغْنِيَ عَنْهُمْ أَمْوَالُهُمْ وَلَا
أَوْلَادُهُم مِّنَ اللَّهِ شَيْئًا ۖ وَأُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۚ
هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿١١٦﴾

117. Mfano wa vile wanavyovitoa katika uhai (wao huu) wa duniani (wakataraji thawabu) ni kama upepo ambao ndani yake mna baridi kali; ukasibu shamba la watu waliodhulumu nafsi zao ukaliangamiza. Na Mwenyezi Mungu hakuwadhulumu, bali wao wenyewe wanadhulumu nafsi zao.

مَثَلُ مَا يُنفِقُونَ فِي هَٰذِهِ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا كَمَثَلِ
رِيحٍ فِيهَا صِرٌّ أَصَابَتْ حَرْثَ قَوْمٍ ظَلَمُوا
أَنفُسَهُمْ فَأَهْلَكَتْهُ ۚ وَمَا ظَلَمَهُمُ اللَّهُ وَلَٰكِنْ
أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿١١٧﴾

118. Enyi mlioamini! Msiwafanye wasiri wenu watu wasiokuwa katika nyinyi: hao hawataacha kukufanyieni ubaya. Wanayapenda yale yanayokudhuruni. Bughudha (yao juu yenu) inadhihirika katika midomo yao. Na yanayofichwa na vifua vyao ni makubwa zaidi. Tumekubainishieni dalili (zote) ikiwa nyinyi ni watu wa kufahamu.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا بِطَانَةً مِّن دُونِكُمْ
لَا يَأْلُونَكُمْ خَبَالًا وَدُّوا مَا عَنِتُّمْ قَدْ بَدَتِ
الْبَغْضَاءُ مِنْ أَفْوَاهِهِمْ وَمَا تُخْفِي صُدُورُهُمْ
أَكْبَرُ ۚ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الْآيَاتِ ۖ إِن كُنتُمْ
تَعْقِلُونَ ﴿١١٨﴾

119. Oh! Nyinyi mnawapenda (maadui zenu hao), hali wao hawakupendeni! Nanyi mnaamini vitabu vyote (chenu na vyao). Na wanapokutana nanyi husema, "Tumeamini". Lakini wanapokuwa peke yao wanakuumieni vyanda kwa uchungu (wa kukuchukieni). Sema: "Kufeni kwa uchungu wenu (huo); hakika Mwenyezi Mungu anayajua (hata) yaliyomo vifuani."

هَا أَنتُمْ أُولَاءِ تُحِبُّونَهُمْ وَلَا يُحِبُّونَكُمْ
وَتُؤْمِنُونَ بِالْكِتَابِ كُلِّهِ وَإِذَا لَقُوكُمْ قَالُوا آمَنَّا
وَإِذَا خَلَوْا عَضُّوا عَلَيْكُمُ الْأَنَامِلَ مِنَ الْغَيْظِ ۚ قُلْ
مُوتُوا بِغَيْظِكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿١١٩﴾

120. Ikikupateni kheri huwasikitisha. Na ikikupateni shari wanaifurahia. Na kama nyinyi mkisubiri na mkamcha Mungu hila zao hazitakudhuruni kitu. Hakika Mwenyezi Mungu anayajua vizuri yote wanayoyatenda.

إِن تَمْسَسْكُمْ حَسَنَةٌ تَسُؤْهُمْ وَإِن تُصِبْكُمْ سَيِّئَةٌ
يَفْرَحُوا بِهَا ۖ وَإِن تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا لَا يَضُرُّكُمْ
كَيْدُهُمْ شَيْئًا ۗ إِنَّ اللَّهَ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ﴿١٢٠﴾

---

117. Ama asiyemkubali Mwenyezi Mungu wala amri Zake na makatazo Yake, hata akifanya mema hana jaza huko Akhera. Akistahiki kulipwa atalipwa papa hapa tu basi.

118. Katika jambo kubwa kabisa linaloongoza mambo ya watu yakaongoka ni kuyapanga na kuyatengeneza kwa siri, yaonekane yamekwisha kusimama; kwani kuna waovu wengi, hawapendi ya wenzao yanyoke, basi mara huyatilia kila namna ya miunda; tahamaki yamepwelewa papo hapo, hayawezi kwenda mbele.

Ndio ikakatazwa hapa kuwafanya wasiokuwa Waislamu kuwa wasiri wenu wa kuwapa habari zenu za ndani. Ama urafiki wa 'Hujambo Sijambo' haukatazwi; wala kuwafanyia mema na insafu, kama yalivyobainishwa haya katika Aya ya 8 ya *Suratul Mumtahina*.

120. Hapa wanaambiwa Waislamu wasiogope uchawi wala marogo wala yaliyo kama haya; bali wamtegemee Mwenyezi Mungu basi. Alitakalo Mwenyezi Mungu kuwa, hakuna awezae kulizuia. Basi nautue moyo wako ukitaka kufanya lako; usimwogope mchawi wala mwanga wala hasidi wala adui. Mlimkiroga na kushiriki, Liwe jambo hilo halifanyiki. Andikalo Mola halifutiki: Hebu lifuteni nasi tuone.

| | |
|---|---|
| Wakanyeni wakanyike | Mahayawani |
| Wanatia usalata | Mitaani |
| Nguvu zao na Za Mola | Bora nani? |
| Wakikushituwa | Wewe sishituke |
| Yupi awezaye | Kupitisha lake |
| Wakiwa na lao | Mungu ana Yake |

وَإِذْ غَدَوْتَ مِنْ أَهْلِكَ تُبَوِّئُ الْمُؤْمِنِينَ مَقَاعِدَ
لِلْقِتَالِ ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿١٢١﴾

121. Na (kumbuka) ulipotoka asubuhi, ukaacha watu wako, ili uwatengenezee Waislamu mahali pa kupigania; na Mwenyezi Mungu anasikia na anajua

إِذْ هَمَّتْ طَائِفَتَانِ مِنْكُمْ أَنْ تَفْشَلَا وَاللَّهُ
وَلِيُّهُمَا ۗ وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٢٢﴾

122. (Kumbuka) makundi mawili miongoni mwenu yalipodhamiria kufanya woga (na kwenda zake kama walivyokwenda zao wale wanafiki). Na Mwenyezi Mungu akawa mlinzi wa yote mawili hayo. (Kwa hivyo yakahifadhika, hayakufanya mabaya hayo). Na Waislamu wamtegemee Mwenyezi Mungu (tu basi).

وَلَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ بِبَدْرٍ وَأَنْتُمْ أَذِلَّةٌ ۖ
فَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٢٣﴾

123. Na Mwenyezi Mungu alikunusuruni katika (vita vya) Badri, hali nyinyi mlikuwa dhaifu. Basi mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kushukuru (kila wakati kwa neema zinazokujieni).

إِذْ تَقُولُ لِلْمُؤْمِنِينَ أَلَنْ يَكْفِيَكُمْ أَنْ يُمِدَّكُمْ
رَبُّكُمْ بِثَلَاثَةِ آلَافٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ مُنْزَلِينَ ﴿١٢٤﴾

124. (Alikunusuruni katika vita vya Badr) ulipowaambia Waislamu: "Je! Haitakutosheni Mola wenu atapokusaidieni kwa Malaika elfu tatu watakaoteremshwa?"

بَلَىٰ ۚ إِنْ تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا وَيَأْتُوكُمْ مِنْ فَوْرِهِمْ
هَٰذَا يُمْدِدْكُمْ رَبُّكُمْ بِخَمْسَةِ آلَافٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ
مُسَوِّمِينَ ﴿١٢٥﴾

125. Naam. Kama mkisubiri na kujilinda na makatazo yake na (maadui) wakakufikieni haraka (kwa shindo), hapo Mola wenu atakusaidieni kwa Malaika elfu tano washambuliao kwa nguvu.

وَمَا جَعَلَهُ اللَّهُ إِلَّا بُشْرَىٰ لَكُمْ وَلِتَطْمَئِنَّ
قُلُوبُكُمْ بِهِ ۗ وَمَا النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ
الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ﴿١٢٦﴾

126. Na Mwenyezi Mungu hakufanya haya (ya kukuleteeni Malaika) ila kuwa bishara kwenu, ili nyoyo zenu zipate kutulia kwayo. Na msaada hautoki (kwa mwengine yo yote) isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu na Mwenye hikima

لِيَقْطَعَ طَرَفًا مِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَوْ يَكْبِتَهُمْ
فَيَنْقَلِبُوا خَائِبِينَ ﴿١٢٧﴾

127. (Kafanya haya ya kukunusuruni) ili akate sehemu katika wale waliokufuru (awaue), au awadhalilishe ili wapate kurudi, na hali wameshindwa.

---

121. Hapa inatajwa habari ya vita vya pili vikubwa kabisa vya Kiislamu (vita vya Uhudi). Katika vita hivi walipata hasara pevu Waislamu kwa ajili ya wale Waislamu wa kweli wachache waliokhalifu amri ya Mtume; na kwa ajili ya wale Waislamu wanafiki waliomfuata Mtume; kisha walipofika vitani wakakimbia. Na walikuwa thuluthi ya jeshi la Uislamu. Basi walikuwa wengi zaidi kuliko hivi, lakini wengine walirejea tena upande wa Waislamu.

124. Hapa inatajwa kwamba Waislamu katika vita vyao na makafiri wakisaidiwa na Malaika makundi kwa makundi. Malaika hawa wakija kwa sura za Kibinadamu na wakipigana kwa nguvu za Kibinadamu. Lau wangekuja Kimalaika, hata mmoja tu angewamaliza makafiri wote.

127, 128. Hapa anataja Mwenyezi Mungu sababu ya kuwaletea nusura, na anaonyesha ufalme Wake; kuwa alitakalo Yeye ndilo Atakalolifanya; si alitakalo Bwana Fulani wala Bwana Fulani, hata akiwa Mtume Muhammad. Basi waongo hao wanaosema kuwa alitakalo Sharifu wao na Sheikh wao au Khalifa wao ndilo litakalokuwa, basi si kweli. Ya kweli ni haya:-

Mambo yote ni ya Mungu
Atakalo ndilo huwa
Ndiye pweke Mwenye quwa
Mwenye amri na shani.

128. Wewe huna lako katika shauri hii — au (Mwenyezi Mungu) awaonee huruma au awaadhibu, maana wao ni madhalimu. (Atafanya anavyoona Mwenyewe).

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ أَوْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ أَوْ يُعَذِّبَهُمْ فَإِنَّهُمْ ظَالِمُونَ ﴿١٢٨﴾

129. Na ni vya Mwenyezi Mungu tu vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; humsamehe amtakaye na humwadhibu amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۚ يَغْفِرُ لِمَنْ يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَنْ يَشَاءُ ۚ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٢٩﴾

130. Enyi mlioamini! Msile riba, mkizidishazidisha; na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kutengenekewa.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَأْكُلُوا الرِّبَا أَضْعَافًا مُضَاعَفَةً ۖ وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿١٣٠﴾

131. Na ogopeni moto ambao umewekewa wenye kukanusha amri za Mwenyezi Mungu. (Na katika hizo ni huku kutokula riba).

وَاتَّقُوا النَّارَ الَّتِي أُعِدَّتْ لِلْكَافِرِينَ ﴿١٣١﴾

132. Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume ili mpate kurehemewa.

وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿١٣٢﴾

133. Na yaendeeni upesi upesi maghufira ya Mola wenu na Pepo (yake) ambayo upana wake (tu) ni (sawa na) mbingu na ardhi. (Pepo) iliyowekewa wamchao Mungu

وَسَارِعُوا إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِنْ رَبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا السَّمَاوَاتُ وَالْأَرْضُ أُعِدَّتْ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٣٣﴾

---

130. Moja katika ubaya wa riba ni kule kuzidi na kuzidi mpaka ikamaliza mali ya mwenzio yote au mengi kabisa, bure kwa unyonge tu na kumwonea. Ndiyo maana ikatajwa katika Aya ya pili (131) kuwa ikiwa hao madhalimu wala riba hawatawacha dhulma yao hiyo na wakarejeza haki za watu, basi Moto wa Jahannam unawangojea tu:

| | |
|---|---|
| Salil Jahimu | Mambo mazito |
| Siyahi na zite | Katika Moto |
| Sura uwakao | Kwa mivukuto |
| Na kwenda miteo | Na kugoroma |
| Dhamirini mwako | Usisahau |
| Dhiki za Motoni | Ukadharau |
| Dhurubu mithali | Kama hiyau |
| Wadhurubiyeo | Wote Ulama |
| Dhalimu wa huku | Ulimwenguni |
| Dhili ya Arishi | Haketi tini |
| Dhulma humpa | Kwenda Motoni |
| Nyumba ya adhabu | Zisizokoma |

132. Na hapa inabainishwa kuwa Rehema ya Mwenyezi Mungu haiwezi kupatikana ila kwa KUMTII Mwenyezi Mungu na Mtume Wake: Kwa kufuata amri zao kiasi cha uweza wako na kuwacha makatazo Yao kabisa kabisa.

Haipatikani Pepo kwa kuwa wewe ni Mwislamu tu (Mwislamu jina), wala kuwa unafuata Madhehebu fulani ya Kiislamu au Tarika fulani; kwa kuwa mkubwa wa madhehebu hayo au mkubwa wa Tarika hiyo atakushufaia. Mtume mwenyewe hatashufaia waliodidimia katika maasi, seuze wengineo.

| | |
|---|---|
| Sharia husema | Aso thawabu |
| Shida na mashaka | Yatamsibu |
| Shufaa ya Tumwa | Lmahbubu |
| Huwa mbali naye | Na kumwegema |

Ameyabainisha Mwenyezi Mungu haya katika Aya ya 1 2 ya *Suratun Nisaa* kama itakavyokuja Inshallah katika tafsiri ya Juzuu ya Sita na kama ilivyobainishwa katika Aya ya 81 ya *Suratul Baqarah*.

133. Aya hii inahimiza watu kufanya upesi upesi mambo ya kuwapatishia radhi za Mwenyezi Mungu na Pepo Yake.

134. Ambao hutoa katika (hali ya) wasaa na katika (hali ya) dhiki, na wazuiyao ghadhabu na wasamehe watu (na wawafanyiao ihsani); na Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao ihsani.

الَّذِينَ يُنفِقُونَ فِي السَّرَّاءِ وَالضَّرَّاءِ
وَالْكَاظِمِينَ الْغَيْظَ وَالْعَافِينَ
عَنِ النَّاسِ ۗ وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٣٤﴾

135. Na ambao wanapofanya uchafu (kufanya dhambi kubwa) au kudhulumu nafsi zao (kwa dhambi ndogo) hukumbuka Mwenyezi Mungu na kuomba msamaha kwa dhambi zao. Na nani anayeghufiria dhambi isipokuwa Mwenyezi Mungu? Na hawaendelei na (maovu) waliyoyafanya, hali wanajua (kuwa hayo ni maovu).

وَالَّذِينَ إِذَا فَعَلُوا فَاحِشَةً أَوْ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ
ذَكَرُوا اللَّهَ فَاسْتَغْفَرُوا لِذُنُوبِهِمْ وَمَن
يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا اللَّهُ وَلَمْ يُصِرُّوا عَلَىٰ
مَا فَعَلُوا وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿١٣٥﴾

136. Hao ndio ambao malipo yao yatakuwa msamaha kwa Mola wao na Bustani (Pepo) zinazopita mito mbele yake, ambamo watakaa milele. Na ni wema ulioje ujira wa watendao (mema).

أُولَٰئِكَ جَزَاؤُهُم مَّغْفِرَةٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَجَنَّاتٌ
تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۚ
وَنِعْمَ أَجْرُ الْعَامِلِينَ ﴿١٣٦﴾

137. Zimepita adabu namna kwa namna walizotiwa waliokuwa kabla yenu. Basi safirini katika nchi na mwone ulikuwaje mwisho wa wale waliokadhibisha.

قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِكُمْ سُنَنٌ فَسِيرُوا فِي
الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكَذِّبِينَ ﴿١٣٧﴾

138. Haya ni maelezo yaliyo wazi kwa watu (wote) na uwongozi na mauidha kwa wamchao.

هَٰذَا بَيَانٌ لِّلنَّاسِ وَهُدًى وَمَوْعِظَةٌ
لِّلْمُتَّقِينَ ﴿١٣٨﴾

139. Na msilegee . wala msihuzunike, maana nyinyi ndio mtakaokuwa juu ikiwa mnaamini kweli.

وَلَا تَهِنُوا وَلَا تَحْزَنُوا وَأَنتُمُ الْأَعْلَوْنَ إِن كُنتُم
مُّؤْمِنِينَ ﴿١٣٩﴾

140. Kama yamekupateni majaraha, basi na watu hao yamewapata majaraha kama haya. Na siku za namna hii tunawaletea watu kwa zamu. (Amefanya haya) ili Mwenyezi Mungu apambanue walioamini (kweli, kwa hivyo hawakukimbia) na afanye miongoni mwenu mashahidi (waliouawa katika hivyo vita wapate daraja ya Ushahidi). Na Mwenyezi Mungu hawapendi madhalimu

إِن يَمْسَسْكُمْ قَرْحٌ فَقَدْ مَسَّ الْقَوْمَ قَرْحٌ مِّثْلُهُ ۚ
وَتِلْكَ الْأَيَّامُ نُدَاوِلُهَا بَيْنَ النَّاسِ وَلِيَعْلَمَ
اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا وَيَتَّخِذَ مِنكُمْ شُهَدَاءَ ۗ
وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ الظَّالِمِينَ ﴿١٤٠﴾

141. Na ili Mwenyezi Mungu awasafishe walioamini na kuwafuta (waondoke ulimwenguni wale) waliokufuru.

وَلِيُمَحِّصَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا وَيَمْحَقَ
الْكَافِرِينَ ﴿١٤١﴾

142. Je! Mnadhani mtaingia Peponi, hali Mwenyezi Mungu hajawapambanua wale waliopigania dini ya Mwenyezi Mungu miongoni mwenu, na kuwapambanua waliofanya subira? (Sharti yaonekane kwanza haya hapa ulimwenguni).

أَمْ حَسِبْتُمْ أَن تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَعْلَمِ اللَّهُ
الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنكُمْ وَيَعْلَمَ الصَّابِرِينَ ﴿١٤٢﴾

---

134-135. Aya hizi zinataja baadhi ya sifa ambazo mtu akisifika nazo ataingia Peponi . . .

140. Wanakumbushwa misukosuko iliyowafika siku ya vita vya Uhudi, na kuwa kama walivyosibiwa wao ndivyo wao nao walivyowasibu maadui zao; na kuwa mambo ndivyo vivi hivi, kwa noba — mara wanapata hawa mara wanapata wale, kwa mujibu wa amali zao, sio Mungu anapendelea.

141-142. Aya hizi na nusu ya Aya ya 140 zinaonyesha sababu za kuwaachilia Mwenyezi Mungu Waislamu washindwe siku hiyo ya vita vya Uhudi.

143. Na nyinyi mlikuwa mkitamani mauti, (kuwa shahidi), kabla hamjakutana nayo. Basi mmekwisha yaona na huku mnayatazama.

وَلَقَدْ كُنتُمْ تَمَنَّوْنَ الْمَوْتَ مِن قَبْلِ أَن
تَلْقَوْهُ فَقَدْ رَأَيْتُمُوهُ وَأَنتُمْ تَنظُرُونَ ﴿١٤٣﴾

144. Na hakuwa Muhammad ila ni Mtume tu. Wamepita kabla yake Mitume (wengi kabisa). Akifa au akiuawa ndiyo mtarudi nyuma (kwa visigino vyenu), muwe makafiri kama zamani? Na atakayerudi nyuma kwa visigino vyake hatamdhuru Mwenyezi Mungu cho chote. Na Mwenyezi Mungu atawalipa wanaomshukuru

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهِ
الرُّسُلُ أَفَإِن مَّاتَ أَوْ قُتِلَ انقَلَبْتُمْ عَلَىٰ
أَعْقَابِكُمْ وَمَن يَنقَلِبْ عَلَىٰ عَقِبَيْهِ فَلَن
يَضُرَّ اللَّهَ شَيْئًا وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ ﴿١٤٤﴾

145. Na nafsi yo yote haitaweza kufa ila kwa amri ya Mwenyezi Mungu kwa ajali iliyowekwa. Na anayetaka malipo ya duniani tutampa, basi, hapa; na anayetaka malipo ya Akhera tutampa huko; na kwa yakini tutawalipa wanaoshukuru.

وَمَا كَانَ لِنَفْسٍ أَن تَمُوتَ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ كِتَابًا
مُّؤَجَّلًا وَمَن يُرِدْ ثَوَابَ الدُّنْيَا نُؤْتِهِ مِنْهَا
وَمَن يُرِدْ ثَوَابَ الْآخِرَةِ نُؤْتِهِ مِنْهَا وَسَنَجْزِي
الشَّاكِرِينَ ﴿١٤٥﴾

146. Na Manabii wangapi walipigana na maadui; na pamoja nao kulikuwa na watakatifu wengi. Hawakulegea kwa yale yaliyowasibu

وَكَأَيِّن مِّن نَّبِيٍّ قَاتَلَ مَعَهُ رِبِّيُّونَ

---

143. Waislamu kwa kusikia fadhila kubwa watakazozipata wanaokufa vitani (Mashahidi), kila mmoja alitamani apate daraja hiyo; basi wameipata. Wameuawa watu 70 mara moja siku ya vita vya Uhudi katika watu 700 waliosimama kupigana na jeshi la watu 3000.

144. Hapa wanajulishwa wazi wazi (wasisahau) kuwa Nabii Muhammad ni Mtume tu ambaye ni kiumbe kama viumbe vyengine—atakufa kama walivyokufa na wanavyokufa.

Basi hata akifa washikane na mwendo huo huo aliowafundisha, wa dini ya haki ya Uislamu. Siyo warejee ukafirini kama zamani kwa kuona kuwa Mtume kafa, basi na mambo yake yamekufa. Isiwe hivyo.

Sababu ya kutajwa visigino hapa ni kuonyesha ule mwendo wa mwenye kurejea nyuma unavyokuwa; lakini hapana visigino hapa wala cho chote.

Watu wengine kwa kutaka kushinda katika ubishi wao wa kuwa Nabii Isa kafa, wameipotoa tafsiri ya *Khalat* wakasema "wamekwisha fariki" yaani wamekwisha kufa. Na hali ya kuwa wanajua — wafasiri hao — kuwa tamko la *khalaa* halifasiriwi kwa kufa; linafasiriwa kwa kuwa "hayupo hapo, au hayuko saa hiyo au patupu hapo, hapana kitu." Nawafunuwe tafsiri zote hizo za Quran walizozitaja mwanzo wa tafsiri yao — kuonyesha kuwa wamefuata tafsiri hizo. Nawatuonyeshe moja katika hiyo iliyofasiri tamko la *khalat* = *Maatat* = kafa. Kabisa hawataiona. Na wanajua yakini kuwa hamna; lakini wanataka kudanganya kama ilivyo ada yao ya kudanganya. Na vile vile mwanzo wa tafsiri yao walitaja vitabu vya kufasiri maneno magumu ya Quran, kama *Al Mufradat*. Nawatazame humo kama wataiona hii *Khalat* imefasiriwa kwa "*Maatat*" au "*Khalàa*" yo yote ile. Na wametaja katika mwanzo wa tafsiri yao makamusi yanayofasiri lugha ya Kiarabu kama *Al Qamus*. Nawatazame humo kama wataona tamko la *khalaa* limefasiriwa kwa *Maata* au *khalat* hii iliyomo katika Quran kuwa imefasiriwa kwa *Maatat*. Bali hata Makamusi ya Kiarabu waliyoyataja wao yasiyotungwa na Waislamu kama Munjid; nayo pia hayakufasiri *khalaa* = *Maata* = *Kafa*. Waongo kabisa. Hawajali hata chembe kusema uwongo wanapotaka kuvutia wayatakayo. Tusiwasadiki kwa lo lote lile wanalolisema hata *Laa Ilaaha Illal Laahu Muhammadur Rasuulul Laah*—kwani wanaifasiri *Rasuulul Laah* kwa maana nyingine siyo ile wanayoiamini Waislamu kama walivyoambiwa na Mwenyewe Mwenyezi Mungu na Mtumewe. Ibilisi anafurahi nao sana sana kwa uhodari wao wa kutokuwa na chembe ya haya katika kule kutaka kwao kupoteza. Wasiokuwa na haya—zamani walikuwa — wana mji wao, lakini sasa wametujia katika miji yetu; bila ya chembe ya Zaibaki ya haya kuwa nayo.

Wamejidai kuandika kuwa: "Mwenyezi Mungu aliteremsha Aya hiyo isemayo kuwa Muhammad s.a.w. ni Mtume, akifa si neno kwani Ma nabii waliomtangulia wamekwisha kufa.' Waongo wakubwa Mwenyezi Mungu hakutumia hapa tamko la kufa — wamepachikia wao tu kwa uwongo wao. Basi tafsiri hiyo ya kufa waliyoitia katika Aya hii na maelezo yao ni mpachiko wao tu walioutia bila ya kuona vibaya.

145. Hapa tunahimizwa tushughulikie zaidi malipo ya Akhera kwani ndiyo yenye kudumu.

146. Wanatiwa moyo Waislamu kuwa wasife nyoyo kukitokea kushindwa kwani ndio mitihani hiyo ya kuzidi kuwatengeneza.

katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawakudhoofika wala hawakudhalilika. Na Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao subira.

147. Wala haikuwa kauli yao (watakatifu hao) ila ni kusema: "Mola wetu! Tughufirie madhambi yetu na kupita kwetu kiasi katika mambo yetu na ithibitishe miguu yetu na utusaidie juu ya watu makafiri."

148. Akawapa Mwenyezi Mungu malipo ya duniani na malipo mazuri ya Akhera. Na Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao mema.

149. Enyi mlioamini! Ikiwa mtawatii waliokufuru watakurudisheni nyuma (katika ukafiri wenu wa zamani) na mtakuwa wenye kukhasirika.

150. Bali Mwenyezi Mungu ndiye Mola wenu; naye ndiye bora (kabisa) katika wasaidizi. (Hapana kama yeye).

151. Tutatia khofu katika nyoyo za wale waliokufuru, kwa sababu ya kumshirikisha kwao Mwenyezi Mungu na (wale waungu wao wa batili) ambao hakuteremsha dalili (ya uungu wao). Na makazi yao yatakuwa Motoni, na ni mabaya yalioje maskani ya madhalimu.

152. Na Mwenyezi Mungu alikukamilishieni miadi yake (ya kuwa mtawashinda). Basi mkawaua kwa idhini yake. Mpaka mliporegea na mkagombana katika shauri lile na mkaasi baada ya yeye kukuonyesheni mliyoyapenda; (hapo ndipo alipoacha kukunusuruni). Wako miongoni mwenu wanaopenda dunia, na wako miongoni mwenu wanaopenda Akhera. Kisha (Mwenyezi Mungu) akakuekeni mbali nao (hao makafiri; msiweze kuwashinda) ili akutieni adabu. Naye sasa amekusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye ihsani nyingi juu ya wanaoamini.

كَثِيرٌ فَمَا وَهَنُوا لِمَا أَصَابَهُمْ فِي
سَبِيلِ اللَّهِ وَمَا ضَعُفُوا وَمَا اسْتَكَانُوا وَاللَّهُ
يُحِبُّ الصَّابِرِينَ ﴿١٤٦﴾
وَمَا كَانَ قَوْلَهُمْ إِلَّا أَنْ قَالُوا رَبَّنَا
اغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا وَإِسْرَافَنَا فِي أَمْرِنَا
وَثَبِّتْ أَقْدَامَنَا وَانْصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ
الْكَافِرِينَ ﴿١٤٧﴾
فَآتَاهُمُ اللَّهُ ثَوَابَ الدُّنْيَا وَحُسْنَ ثَوَابِ
الْآخِرَةِ وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٤٨﴾
يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنْ تُطِيعُوا الَّذِينَ كَفَرُوا
يَرُدُّوكُمْ عَلَى أَعْقَابِكُمْ فَتَنْقَلِبُوا خَاسِرِينَ ﴿١٤٩﴾
بَلِ اللَّهُ مَوْلَاكُمْ وَهُوَ خَيْرُ النَّاصِرِينَ ﴿١٥٠﴾
سَنُلْقِي فِي قُلُوبِ الَّذِينَ كَفَرُوا الرُّعْبَ بِمَا
أَشْرَكُوا بِاللَّهِ مَا لَمْ يُنَزِّلْ بِهِ سُلْطَانًا
وَمَأْوَاهُمُ النَّارُ وَبِئْسَ مَثْوَى الظَّالِمِينَ ﴿١٥١﴾
وَلَقَدْ صَدَقَكُمُ اللَّهُ وَعْدَهُ إِذْ تَحُسُّونَهُمْ
بِإِذْنِهِ حَتَّى إِذَا فَشِلْتُمْ وَتَنَازَعْتُمْ فِي الْأَمْرِ
وَعَصَيْتُمْ مِنْ بَعْدِ مَا أَرَاكُمْ مَا تُحِبُّونَ
مِنْكُمْ مَنْ يُرِيدُ الدُّنْيَا وَمِنْكُمْ مَنْ يُرِيدُ
الْآخِرَةَ ثُمَّ صَرَفَكُمْ عَنْهُمْ لِيَبْتَلِيَكُمْ وَلَقَدْ
عَفَا عَنْكُمْ وَاللَّهُ ذُو فَضْلٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٥٢﴾

---

147. Katika Aya waliyoifanya ya 148 wameandika hivi: "Kwa maana ya neno kughofiri dhambi, tazama Sura 48:3; 11:48 na 38:24." Tutajibu Inshallah hapo tutapofika Sura hizi ikistahiki kujibiwa. Ya nini kutafuta Mbeleko kabla ya Mwana kuzaliwa.

151. Hapa Mwenyezi Mungu anawaahidi Waislamu kuwa atawatia khofu wale maadui zao — waliokwisha kwenda zao baada ya kule kushinda kwao — kuwa hawatarejea kuwapiga.

152. Wanatajiwa sababu iliyowapelekea kushindwa. Nayo ni kukhalifu amri ya Mtume aliyowapa . . .
Mtume aliwaweka watu 50 katika jabali; ambao walikuwa mahodari kwa kupiga mishare (mishale). Akawaambia wakae hapo, wawahami, yasije majeshi ya Maqureshi kuwashambulia kwa nyuma. Wawe tayari kuwapiga barabara kwa mishare wakiwajia kwa nyuma. Akawaambia wasiondoke hata ikiwa nini, hata wakiwaona wenzao wameshinda au wameshindwa. Wasiondoke mpaka mkubwa wao aletewe amri na Mtume ya kuondoka.

Lakini baadhi yao — isipokuwa watu 14 tu — walikhalifu amri hii walipowaona wenziwao wameshinda kweli

153. (Kumbukeni) mlipokuwa mkikimbia mbio, wala nyinyi hamumsikilizi yo yote, hali Mtume alikuwa anakwiteni, yuko nyuma yenu. Akakupeni (Mwenyezi Mungu) huzuni juu ya huzuni. (Amekusameheni hivyo) ili msisikitike (sana) kwa yale yaliyokupoteeni wala kwa (misiba) iliyokusibuni. Na Mwenyezi Mungu ana khabari za yote mnayoyatenda.

إِذْ تُصْعِدُونَ وَلَا تَلْوُونَ عَلَىٰٓ أَحَدٍ وَ
ٱلرَّسُولُ يَدْعُوكُمْ فِىٓ أُخْرَىٰكُمْ فَأَثَٰبَكُمْ
غَمًّۢا بِغَمٍّ لِّكَيْلَا تَحْزَنُوا۟ عَلَىٰ مَا فَاتَكُمْ
وَلَا مَآ أَصَٰبَكُمْ ۗ وَٱللَّهُ خَبِيرٌۢ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٥٣﴾

154. Kisha baada ya huzuni alikuteremshieni utulivu — usingizi ambao ulifunika kundi moja katika nyinyi. Na kulikuwa kundi jengine nafsi zao zimewashughulisha (hawajijui hawajitambui); wakimdhania Mwenyezi Mungu dhana zisizokuwa ndizo, dhana za ujinga; wakisema. "Ah! Tuna amri sisi katika jambo hili?" Sema: "Mambo yote ni ya Mwenyezi Mungu." Wanaficha katika roho zao (hao wanafiki) wasiyokubainishia. Wanasema: "Tungekuwa na cho chote katika jambo hili tusingeuawa hapa." Sema: "Hata mngalikuwa majumbani mwenu, basi wangalitoka wale walioandikiwa kufa, wakenda mahali pao pa kuangukia wafe. (Amefanya haya Mwenyezi Mungu ili) ayadhihirishe yaliyomo vifuani mwenu, na asafishe yaliyo nyoyoni mwenu. Na Mwenyezi Mungu anayajua (hata) yaliyomo vifuani.

ثُمَّ أَنزَلَ عَلَيْكُم مِّنۢ بَعْدِ ٱلْغَمِّ أَمَنَةً
نُّعَاسًا يَغْشَىٰ طَآئِفَةً مِّنكُمْ ۖ وَطَآئِفَةٌ قَدْ
أَهَمَّتْهُمْ أَنفُسُهُمْ يَظُنُّونَ بِٱللَّهِ غَيْرَ ٱلْحَقِّ ظَنَّ
ٱلْجَٰهِلِيَّةِ ۖ يَقُولُونَ هَل لَّنَا مِنَ ٱلْأَمْرِ مِن
شَىْءٍ ۗ قُلْ إِنَّ ٱلْأَمْرَ كُلَّهُۥ لِلَّهِ ۗ يُخْفُونَ فِىٓ
أَنفُسِهِم مَّا لَا يُبْدُونَ لَكَ ۖ يَقُولُونَ لَوْ كَانَ
لَنَا مِنَ ٱلْأَمْرِ شَىْءٌ مَّا قُتِلْنَا هَٰهُنَا ۗ قُل لَّوْ
كُنتُمْ فِى بُيُوتِكُمْ لَبَرَزَ ٱلَّذِينَ كُتِبَ عَلَيْهِمُ ٱلْقَتْلُ
إِلَىٰ مَضَاجِعِهِمْ ۖ وَلِيَبْتَلِىَ ٱللَّهُ مَا فِى صُدُورِكُمْ
وَلِيُمَحِّصَ مَا فِى قُلُوبِكُمْ ۗ وَٱللَّهُ عَلِيمٌۢ
بِذَاتِ ٱلصُّدُورِ ﴿١٥٤﴾

155. Wale waliorudi nyuma (waliokimbia) miongoni mwenu siku ambayo majeshi mawili yalipokutana (katika vita vya Uhudi — jeshi la makafiri na Waislamu), Shetani ndiye aliyewatelezesha kwa (sababu ya) baadhi ya (makosa) waliyoyafanya; na Mwenyezi Mungu (sasa) amewasamehe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mpole sana.

إِنَّ ٱلَّذِينَ تَوَلَّوْا۟ مِنكُمْ يَوْمَ ٱلْتَقَى ٱلْجَمْعَانِ
إِنَّمَا ٱسْتَزَلَّهُمُ ٱلشَّيْطَٰنُ بِبَعْضِ مَا كَسَبُوا۟ ۖ
وَلَقَدْ عَفَا ٱللَّهُ عَنْهُمْ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٌ حَلِيمٌ ﴿١٥٥﴾ ع

---

kweli, wanawaendesha mbio Maqureshi na kuwaua na kuwateka na kuchukua mali yao ngawira. Waliteremka wakachanganyika nao katika kule kukusanya ngawira. Mkubwa wao aliwakataza kweli kweli lakini hawakumsikia kabisa isipokuwa wale wachache tu aliosalia nao hapo.

Baadhi ya majamadari wa lile jeshi la Maqureshi lililokuwa likikimbia walipoona wale wanaohami lile jabali hawapo, waligeuza jeshi lao, wakawashambulia Waislamu kwa nyuma. Kikawa kivangaito sasa, wakafa chungu ya waliokufa, na wakajuruhiwa chungu ya waliojuruhiwa.

154. Baada ya kushindwa kule Waislamu, na makafiri wakenda zao, baadhi ya wanafiki waliokuwa katika hilo jeshi la Waislamu (waliokuwa hawajakimbia pamoja na wenzao) hawakuamini kuwa makafiri ndio wamekwenda zao kweli kweli hivyo. Wala hawakuamini ule waadi wa Mwenyezi Mungu kuwa atawatia khofu wasirejee. Waliona kuwa wamekwenda kidogo tu hivi, kisha watarejea kuwasagasaga. Basi usingizi uliwapaa—wasilitungue la mchana wala la usiku. Na wenzao — wale Waislamu wa kweli — wakawa bukheri wa afiya; wanalala na kuamka na kula na kunywa na kuzungumza na kufanya mengineyo.

155. Siku ya vita vya Uhudi — kama tulivyokwishaona–wanafiki 300 walikimbia kabla ya vita havijaanza. Khalafu baadhi ya Waislamu walikhalifu amri ya Mtume pale wakati ambao ilionyesha wazi wazi kuwa wao Waislamu ndio watakaoshinda. Walipokhalifu hivyo mara mambo yaligeuka—ikawa sasa Waislamu wanapigwa na kuuawa; hata ikadhaniwa kuwa Mtume kauawa. Katika mtaharuki huu basi Waislamu wengi—ambao ni Waislamu wazuri kabisa—walikimbia. Walirukwa na akili wakawa hawajui la kufanya. Basi wakakimbia.

156. Enyi mlioamini! Msiwe kama wale waliokufuru na wakasema juu ya ndugu zao waliposafiri katika nchi au walipopigana (wakafa): "Wangalikuwa kwetu wasingalikufa wala wasingaliuawa." (Amewatia Mwenyezi Mungu dhana hii) ili afanye hayo kuwa majuto katika nyoyo zao. Na Mwenyezi Mungu anahuisha na kufisha na Mwenyezi Mungu anaona yote mnayoyatenda.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَكُونُواْ كَٱلَّذِينَ كَفَرُواْ
وَقَالُواْ لِإِخۡوَٰنِهِمۡ إِذَا ضَرَبُواْ فِي ٱلۡأَرۡضِ أَوۡ
كَانُواْ غُزࣰّى لَّوۡ كَانُواْ عِندَنَا مَا مَاتُواْ وَمَا
قُتِلُواْ لِيَجۡعَلَ ٱللَّهُ ذَٰلِكَ حَسۡرَةࣰ فِي قُلُوبِهِمۡۗ وَ
ٱللَّهُ يُحۡيِۦ وَيُمِيتُۗ وَٱللَّهُ بِمَا تَعۡمَلُونَ بَصِيرࣱ ﴿١٥٦﴾

157. Na kama mkiuawa katika njia ya Mwenyezi Mungu au mkifa (si khasara kwenu) kwani msamaha na rehema zinazotoka kwa Mwenyezi Mungu (kukujieni) ni bora kuliko vile wanavyokusanya (hapa ulimwenguni).

وَلَئِن قُتِلۡتُمۡ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ أَوۡ مُتُّمۡ لَمَغۡفِرَةࣱ
مِّنَ ٱللَّهِ وَرَحۡمَةٌ خَيۡرࣱ مِّمَّا يَجۡمَعُونَ ﴿١٥٧﴾

158. Na kama mkifa au mkiuawa (ni sawasawa); (nyote) mtakusanywa kwa Mwenyezi Mungu.

وَلَئِن مُّتُّمۡ أَوۡ قُتِلۡتُمۡ لَإِلَى ٱللَّهِ تُحۡشَرُونَ ﴿١٥٨﴾

159. Basi kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu umekuwa laini kwao (Ewe Muhammad). Na kama ungekuwa mkali na mwenye moyo mgumu bila shaka wangalikukimbia. Basi wasamehe wewe na uwaombee msamaha (kwa Mwenyezi Mungu) na ushauriane nao katika mambo. Na ufungapo nia mtegemee Mwenyezi Mungu (tu ufanye hili uliloazimia). Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wamtegemeyao.

فَبِمَا رَحۡمَةࣲ مِّنَ ٱللَّهِ لِنتَ لَهُمۡۖ وَلَوۡ كُنتَ فَظًّا
غَلِيظَ ٱلۡقَلۡبِ لَٱنفَضُّواْ مِنۡ حَوۡلِكَۖ فَٱعۡفُ
عَنۡهُمۡ وَٱسۡتَغۡفِرۡ لَهُمۡ وَشَاوِرۡهُمۡ فِي ٱلۡأَمۡرِۖ فَإِذَا
عَزَمۡتَ فَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱللَّهِۚ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ
ٱلۡمُتَوَكِّلِينَ ﴿١٥٩﴾

160. Ikiwa Mwenyezi Mungu anakunusuruni, basi hakuna atakayeweza kukushindeni Na kama akikuacheni nani tena atakayekunusuruni baada yake? Basi Waislamu wamtegemee Mwenyezi Mungu tu.

إِن يَنصُرۡكُمُ ٱللَّهُ فَلَا غَالِبَ لَكُمۡۖ وَإِن يَخۡذُلۡكُمۡ
فَمَن ذَا ٱلَّذِي يَنصُرُكُم مِّنۢ بَعۡدِهِۦۗ وَعَلَى ٱللَّهِ
فَلۡيَتَوَكَّلِ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ﴿١٦٠﴾

161. Wala haiwezekani kwa Nabii kufanya khiyana. Na atakayefanya khiyana, atavileta siku ya Kiyama alivyovifanyia khiana, kisha kila mtu atalipwa kwa aliyoyachuma, (kwa ukamilifu); wala hawatadhulumiwa.

وَمَا كَانَ لِنَبِيٍّ أَن يَغُلَّۚ وَمَن يَغۡلُلۡ يَأۡتِ بِمَا
غَلَّ يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِۚ ثُمَّ تُوَفَّىٰ كُلُّ نَفۡسࣲ مَّا
كَسَبَتۡ وَهُمۡ لَا يُظۡلَمُونَ ﴿١٦١﴾

---

Basi hapa Mwenyezi Mungu anasema kuwa kawasamehe; na anawaambia kuwa yamewafika hayo kwa ajili ya makosa yao waliyoyafanya. Ndipo shetani akaweza kuwachezea.

156-157. Wanaliwazwa, wasione kuwa huko kufa kumewapata kwa ajili ya huko kwenda vitani, lau wasingekwenda yasingewapata. Wanaambiwa kuwa wamekufa kwa kuwa muda wao walioandikiwa na Mwenyezi Mungu wa kuishi duniani umekwisha; hata wangekuwa majumbani mwao wangekufa. Na wanabainishiwa kuwa huko kufa vitani ni bora kabisa kwao.

159. Hapa Mwenyezi Mungu anamtia nguvu Mtume kuendelea na sifa yake ya upole na ustahamilivu juu ya yote yale anayofanyiwa na watu. Na anamwonyesha kuwa kupewa upole huo ni rehema kubwa inayotoka kwa Mwenyezi Mungu.

Na anahimizwa Mtume anapotaka kufanya jambo ashauriane na watu wake, asikate mwenyewe tu peke yake kwani kutakana shauri kuna nafuu kubwa. Na anawakataza wasiwe Vigeugeu—wakisha kushauriana wakaona wafanye kitu fulani; basi nawamtegemee Mwenyezi Mungu wakifanye tu kitu hicho; wasitie tena hili wala hili.

161. Hapa inakatazwa mtu kukhini hata kidogo. Hata akiwa ndiye mkubwa wao, hana ruhusa kuchukua kitu japo kidogo pasi na kuwapa habari na kupata ridhaa yao kwanza. Hata mwenyewe Mtume; seuze mtu mwengine. Na kuonyesha kuwa siku ya Kiyama kila mwenye kukhini atakuja na kile alichokichukua kwa khiana; atahayarishwe mbele za umma wote; kisha atiwe Motoni.

162. Je! Aliyeyafuata ya kumridhisha Mwenyezi Mungu ni kama yule aliyestahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na makazi yake yakawa jahannam? Napo ni mahala pabaya pa kurejea (mtu).

أَفَمَنِ اتَّبَعَ رِضْوَانَ اللَّهِ كَمَنْ بَاءَ بِسَخَطٍ مِّنَ
اللَّهِ وَمَأْوَاهُ جَهَنَّمُ ۚ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿١٦٢﴾

163. Hao (viumbe) wana vyeo (mbali mbali) mbele ya Mwenyezi Mungu (kwa mnasaba wa amali zao). Na Mwenyezi Mungu huona yote wanayoyatenda.

هُمْ دَرَجَٰتٌ عِندَ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ بَصِيرٌۢ بِمَا يَعْمَلُونَ ﴿١٦٣﴾

164. Hakika Mwenyezi Mungu amewafanyia hisani kubwa Waislamu alivyowaletea Mtume miongoni mwao, anayewasomea Aya zake, na anawatakasa na kuwafundisha Kitabu na hikima. Na bila shaka kabla ya hapo walikuwa katika upotofu dhahiri.

لَقَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ إِذْ بَعَثَ فِيهِمْ
رَسُولًا مِّنْ أَنفُسِهِمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ ءَايَٰتِهِۦ وَيُزَكِّيهِمْ
وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَٰبَ وَالْحِكْمَةَ وَإِن كَانُوا مِن قَبْلُ
لَفِي ضَلَٰلٍ مُّبِينٍ ﴿١٦٤﴾

النصف

165. Nyinyi — ulipokufikieni msiba ambao nyinyi mmekwisha watia (maadui) mara mbili ya huo — mnasema: "Umetoka wapi huu?" Sema: "Huo umetoka kwenu wenyewe." Hakiaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

أَوَلَمَّا أَصَٰبَتْكُم مُّصِيبَةٌ قَدْ أَصَبْتُم مِّثْلَيْهَا
قُلْتُمْ أَنَّىٰ هَٰذَا ۖ قُلْ هُوَ مِنْ عِندِ أَنفُسِكُمْ ۗ إِنَّ
اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٦٥﴾

166. Na msiba ule uliokufikieni siku ya mkutano wa majeshi mawili (la Waislamu na makafiri) ulikuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu; na kuwapambanua walioamini

وَمَا أَصَٰبَكُمْ يَوْمَ الْتَقَى الْجَمْعَانِ فَبِإِذْنِ اللَّهِ
وَلِيَعْلَمَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٦٦﴾

167. Na kuwapambanua wale waliokuwa wanafiki. Nao waliambiwa: "Njooni mpigane katika njia ya Mwenyezi Mungu au mzuie (maadui pamoja na sisi)". Wakasema: "Tungejua kuwa kuna kupigana bila ya shaka tungelikufuateni." Wao siku ile walikuwa karibu na ukafiri kuliko na Uislamu (japokuwa siku zote wakidhihirisha Uislamu wa uwongo). Wanasema kwa midomo yao yasiyokuwa nyoyoni mwao. Na Mwenyezi Mungu anajua vyema (yote) wanayoyaficha.

وَلِيَعْلَمَ الَّذِينَ نَافَقُوا ۚ وَقِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا
قَٰتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَوِ ادْفَعُوا ۖ قَالُوا لَوْ نَعْلَمُ
قِتَالًا لَّاتَّبَعْنَٰكُمْ ۗ هُمْ لِلْكُفْرِ يَوْمَئِذٍ أَقْرَبُ
مِنْهُمْ لِلْإِيمَٰنِ ۚ يَقُولُونَ بِأَفْوَٰهِهِم مَّا لَيْسَ
فِي قُلُوبِهِمْ ۗ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا يَكْتُمُونَ ﴿١٦٧﴾

---

164. Hapa Mwenyezi Mungu anawakumbusha Waislamu neema kubwa aliyowapa — ya kuwaletea Mtume .... Na kuonyesha kuwa walikuwa katika upotevu mkubwa, na sasa wameingia katika uwongofu mkubwa mno kabisa.

165. Waislamu — kama tulivyoona–walishinda katika vita vya Badri na wakashindwa katika vita vya Uhudi. Basi wakastaajabu wakawa wanaulizana kwa nini kuwafika msiba huo. Lakini wamesahau kuwa walikhalifu amri alizowapa Mtume. Basi wanaambiwa hiyo ndiyo sababu iliyowapelekea kushindwa.

Na wao waliwatia makafiri msiba mkubwa mara mbili kuliko hao makafiri walivyowatia wao (Waislamu). Siku ya vita vya Badri Waislamu waliwaua makafiri 70 na wakawateka 70 na wakapata ngawira kubwa. Na katika siku ya vita vya Uhudi wameuawa Waislamu 70. Lakini hakutekwa hata mmoja wala hakikuchukuliwa chao kwa ngawira.

167. Tumeona kuwa siku ya vita vya Uhudi — kabla ya kuanza kupigana — walikwenda zao wanafiki 300 (Thuluthi ya jeshi la Waislamu). Walipoombwa na Waislamu waje (a) Kupigana kama wao watakavyopigana au waje (b) Kuogeza tu idadi ili kuwatishia maadui walijibu "Tungejua kuwa kuna kupigana tungelikufuateni." Yaani

168. Wale wasliosema juu ya ndugu zao — na (wao wenyewe) wamekataa kwenda (hawakwenda) vitani: "Wangalitutii wasingeuawa." Sema: "Jiondoleeni mauti (nyinyi wenyewe msife maisha) ikiwa mnasema kweli."

الذين قالوا لإخوانهم وقعدوا لو أطاعونا ما قتلوا ۗ قل فادرءوا عن أنفسكم الموت إن كنتم صادقين ﴿١٦٨﴾

169. Wala usiwadhani wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni wafu (maiti). Bali wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao

ولا تحسبن الذين قتلوا في سبيل الله أمواتا ۚ بل أحياء عند ربهم يرزقون ﴿١٦٩﴾

170. Wanafurahia aliyowapa Mwenyezi Mungu kwa fadhila Zake; na wanawashangilia wale ambao hawajajiunga nao, walio nyuma yao, (wako ulimwenguni, bado hawajafa); ya kwamba haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.

فرحين بما آتاهم الله من فضله ويستبشرون بالذين لم يلحقوا بهم من خلفهم ألا خوف عليهم ولا هم يحزنون ﴿١٧٠﴾

171. Wanashangilia neema na fadhila za Mwenyezi Mungu, na kwamba Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa wanaoamini.

يستبشرون بنعمة من الله وفضل وأن الله لا يضيع أجر المؤمنين ﴿١٧١﴾

172. Wale waliomwitikia Mwenyezi Mungu na Mtume baada ya majaraha yaliyowapata; kwa wale waliofanya wema — nao ndio hawa — na kumcha Mungu utakuwa ujira mkubwa.

الذين استجابوا لله والرسول من بعد ما أصابهم القرح ۚ للذين أحسنوا منهم واتقوا أجر عظيم ﴿١٧٢﴾

173. Wale ambao watu (waliokodiwa na Makureshi) waliwaambia (Waislamu): "Watu (yaani Makureshi) wamekukusanyikieni. Kwa hivyo waogopeni." Lakini (maneno hayo) yakawazidishia imani (Waislamu), wakasema: "Mwenyezi Mungu anatutosha (atatukifia). Naye ni Mlinzi bora kabisa."

الذين قال لهم الناس إن الناس قد جمعوا لكم فاخشوهم فزادهم إيمانا وقالوا حسبنا الله ونعم الوكيل ﴿١٧٣﴾

---

"Lakini kuna kufa tu huko; hamwezi kukabiliana na hao maadui zenu waliozatiti kweli kweli na walio zaidi ya mara tatu kuliko nyinyi. Mnakwenda kuziua nafsi zenu."

Basi Mwenyezi Mungu alileta misukosuko hii ili wapambanuke wapi Waislamu wa kweli na wapi wanafiki, ingawa mbele ya Mtume na mbele ya Masahaba wanajifanya Waislamu.

168. Katika kule kurejea kwao wale wanafiki, baadhi ya wanafiki wenziwao hawakurejea, wakapigana pamoja na Waislamu, wakauawa. Basi ndipo wanafiki waliposema "Wangalitutii (wakenda zao kama tulivyokwenda zetu) wasingeuawa." Na Mungu anawavunja hapa kwa kuwaambia "Hebu nyinyi jiondoleeni mauti maisha yenu. Maadam hamwendi vitani basi msife." Kila kitu kikifika ajali yake kitakufa tu, hata juu ya kitanda chake.

169. Aya hii na zifuatazo zinataja mazuri wanayoyapata wanaokufa katika vita vya Uislamu (*Jihadi*). Wanakuwa wahai. Lakini uhai wao si kama huu tunaoujua sisi. Si wa kiduniani huo. Huo ni uhai kamili wa Kiakhera.

172. Baada ya kuuawa wale Waislamu 70 katika vita vya Uhudi na kujuruhiwa vibaya vibaya vile wote waliohudhuria vita hivyo, Mtume aliwaamrisha waondoke hapo hapo na hali yao hiyo hiyo wawafuate wale maadui zao waliowajarihi hivyo. Wakaondoka wakawafuatia. Lakini wale maadui ilipowafikilia habari hiyo, kuwa wanafuatiwa, walidhani wanafuatwa na jeshi kubwa zaidi — silo lile walilolisagasaga. Wakakaza mwendo wakakimbilia kwao; na Waislamu nao wakarejea baada ya kuwafuatia masafa marefu wasiwakute. Walifika mpaka mahala panapoitwa Hamraal Asad.

Basi hapa Mwenyezi Mungu anawasifu Masahaba hawa.

173. Hapa wanatajwa tena Waislamu hawa — na wenziwao waliochanganyika nao baadaye.

Makafiri — baada ya kuwashinda vile Waislamu katika vita vya Uhudi — walimwambia Mtume pale pale katika midani ya vita kuwa wakutane mwakani siku fulani ya mwezi fulani katika uwanja wa Badri kama

174. Basi wakarudi (vitani) na neema za Mwenyezi Mungu na fadhila (zake), hakuna ubaya uliowagusa; na wakafuata yanayomridhisha Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu.

فَانْقَلَبُوا بِنِعْمَةٍ مِّنَ اللّٰهِ وَفَضْلٍ لَّمْ يَمْسَسْهُمْ
سُوْٓءٌ ۙ وَّاتَّبَعُوْا رِضْوَانَ اللّٰهِ ۗ وَاللّٰهُ ذُوْ فَضْلٍ عَظِيْمٍ ﴿۱۷۴﴾

175. Huyo (aliyekutieni khofu ile) ni Shetani ambaye anakugopesheni marafiki zake, basi msiwaogope; bali niogopeni Mimi mkiwa Waislamu (kweli).

اِنَّمَا ذٰلِكُمُ الشَّيْطٰنُ يُخَوِّفُ اَوْلِيَآءَهٗ ۖ فَلَا تَخَافُوْهُمْ
وَخَافُوْنِ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿۱۷۵﴾

176. Wala wasikuhuzunishe wale wanaokimbilia ukafirini (wafanyao haraka kukataa na kukataza watu Uislamu). Hakika hao hawataidhuru (dini ya) Mwenyezi Mungu chochote. Mwenyezi Mungu anataka asiwawekee sehemu yo yote katika Akhera. Na itakuwa kwao adhabu kubwa (kabisa).

وَلَا يَحْزُنْكَ الَّذِيْنَ يُسَارِعُوْنَ فِي الْكُفْرِ ۚ اِنَّهُمْ
لَنْ يَّضُرُّوا اللّٰهَ شَيْـًٔا ۗ يُرِيْدُ اللّٰهُ اَلَّا يَجْعَلَ
لَهُمْ حَظًّا فِي الْاٰخِرَةِ ۚ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيْمٌ ﴿۱۷۶﴾

177. Hakika wale waliokhiari ukafiri kuliko Uislamu hawataweza kuidhuru dini ya Mwenyezi Mungu cho chote; na itakuwa kwao adhabu iumizayo.

اِنَّ الَّذِيْنَ اشْتَرَوُا الْكُفْرَ بِالْاِيْمَانِ لَنْ يَّضُرُّوا
اللّٰهَ شَيْـًٔا ۚ وَلَهُمْ عَذَابٌ اَلِيْمٌ ﴿۱۷۷﴾

178. Wala wasidhani wale wanaokufuru kwamba huu muda tunaowapa (wakaishi kwa starehe) ni bora kwao. Hakika tunawapa muda na (inatokea ya kuwa) wanazidi madhambi (katika muda huo). Na itakuwa kwao adhabu ya kuwadhalilisha.

وَلَا يَحْسَبَنَّ الَّذِيْنَ كَفَرُوْٓا اَنَّمَا نُمْلِيْ لَهُمْ خَيْرٌ
لِّاَنْفُسِهِمْ ۗ اِنَّمَا نُمْلِيْ لَهُمْ لِيَزْدَادُوْٓا اِثْمًا ۚ
وَلَهُمْ عَذَابٌ مُّهِيْنٌ ﴿۱۷۸﴾

179. Haiwi kwa Mwenyezi Mungu kuwaacha Waislamu katika hali mliyo nayo mpaka apambanue wabaya katika wema. Wala haiwi kwa Mwenyezi Mungu kukujulisheni mambo ya ghaibu. Bali Mwenyezi Mungu huchagua katika Mitume wake amtakaye (akamjulisha baadhi ya hayo). Basi mwaminini Mwenyezi Mungu na Mitume yake. Na kama mtaamini na mtamwogopa (Mungu), basi utakuwa kwenu ujira mkubwa.

مَا كَانَ اللّٰهُ لِيَذَرَ الْمُؤْمِنِيْنَ عَلٰى مَآ اَنْتُمْ عَلَيْهِ
حَتّٰى يَمِيْزَ الْخَبِيْثَ مِنَ الطَّيِّبِ ۗ وَمَا كَانَ اللّٰهُ
لِيُطْلِعَكُمْ عَلَى الْغَيْبِ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ يَجْتَبِيْ مِنْ
رُّسُلِهٖ مَنْ يَّشَآءُ ۖ فَاٰمِنُوْا بِاللّٰهِ وَرُسُلِهٖ ۚ وَاِنْ
تُؤْمِنُوْا وَتَتَّقُوْا فَلَكُمْ اَجْرٌ عَظِيْمٌ ﴿۱۷۹﴾

---

walivyokabiliana katika vita vya mwanzo — vya Badri — basi safari hii wakutane Badri tena. Mtume akaitikia.

Hata 'Mwakani' ulipofika, wakawa Waislamu tayari kwenda kukabiliana na maadui zao, Makureshi; hao Makureshi walifanya woga; wakaogopa kutoka kwenda kukabiliana nao. Lakini walichelea kutukanwa na hao Waislamu na kutukanwa na kabila nyengine kuwa 'wamekhalifu miadi, wameogopa, hawakwenda kukabiliana na maadui zao'. Basi waliwakodi watu wakawapeleka Madina kuwatishia Waislamu kuwa "Kuna khatari kubwa huko. Msitoke kwenda kukabiliana na Makureshi. Wamezatiti vibaya kabisa. Asiye mwana aeleke jiwe!"

Lakilni wapi! Propaganda yao hiyo haikuwafazaisha Waislamu; bali walitoka wakawaendea na huku wanasema 'Mwenyezi Mungu anatutosha . . .'

Wakafika huko Badri wasiwakute Makureshi. Wakakutana na Waarabu wengine, wakafanya nao biashara; wakapata faida kubwa. Na Makureshi wakapata jina baya la uoga na kukhalifu waadi.

178. Kutawilika umri wale wabaya ni madhara zaidi kwao kwani yanazidi mabaya yao na itazidi ikabu yao. Kutawilika umri huwa kuzuri kwa watu wema kwani unaongezeka wema wao.

179. Hiyo misukosuko wanayotiwa Waislamu, Mwenyezi Mungu anawatia makusudi ili wapambanuke wapi Waislamu wa kweli (watakaothibiti katika dini juu ya taabu zinazowafika) na wapi Waislamu waongo ambao

180. Wala wasione wale ambao wanafanya ubakhili katika yale aliyowapa Mwenyezi Mungu katika fadhila Zake kuwa ni bora kwao (kufanya ubakhili huko). La, ni vibaya kwao. Watafungwa kongwa (madude ya kunasa shingoni) za yale waliyoyafanyia ubakhili — siku ya Kiyama. Na urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ana khabari za (yote) mnayoyafanya.

وَلَا يَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَبْخَلُونَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِن فَضْلِهِ هُوَ خَيْرًا لَّهُمْ ۖ بَلْ هُوَ شَرٌّ لَّهُمْ ۖ سَيُطَوَّقُونَ مَا بَخِلُوا بِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ وَلِلَّهِ مِيرَاثُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿١٨٠﴾

181. Mwenyezi Mungu amekwisha sikia kauli ya wale (Mayahudi) waliosema: "Mwenyezi Mungu ni fakiri, na sisi ni matajiri." Tumeyaandika haya waliyoyasema, na (tumeandika) kuua kwao Manabii bila ya haki, na tutawaambia (Siku ya Kiyama): "Onjeni adhabu ya kuungua."

لَّقَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ فَقِيرٌ وَنَحْنُ أَغْنِيَاءُ ۘ سَنَكْتُبُ مَا قَالُوا وَقَتْلَهُمُ الْأَنبِيَاءَ بِغَيْرِ حَقٍّ وَنَقُولُ ذُوقُوا عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿١٨١﴾

182. "Haya ni kwa sababu ya yale iliyoyatanguliza mikono yenu, na kwamba Mwenyezi Mungu si dhalimu kwa watumwa (wake)."

ذَٰلِكَ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيكُمْ وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿١٨٢﴾

183. Wale waliosema: "Mwenyezi Mungu ametuahidi ya kwamba tusiamini Mtume yo yote mpaka atuletee kafara ambayo huliwa na moto." Sema: "Walikufikieni Mitume kabla yangu kwa hoja zilizo wazi na kwa haya mnayosema. Basi mbona mliwaua, kama mlikuwa wakweli?"

الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ عَهِدَ إِلَيْنَا أَلَّا نُؤْمِنَ لِرَسُولٍ حَتَّىٰ يَأْتِيَنَا بِقُرْبَانٍ تَأْكُلُهُ النَّارُ ۗ قُلْ قَدْ جَاءَكُمْ رُسُلٌ مِّن قَبْلِي بِالْبَيِّنَاتِ وَبِالَّذِي قُلْتُمْ فَلِمَ قَتَلْتُمُوهُمْ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٨٣﴾

184. Na kama wakikukadhibisha (Ewe Muhammad), basi (si ajabu, kwani) walikadhibishwa Mitume kabla yako waliofika na hoja waziwazi na Vitabu vyenye hikima, na Vitabu vyenye nuru.

فَإِن كَذَّبُوكَ فَقَدْ كُذِّبَ رُسُلٌ مِّن قَبْلِكَ جَاءُوا بِالْبَيِّنَاتِ وَالزُّبُرِ وَالْكِتَابِ الْمُنِيرِ ﴿١٨٤﴾

---

hawataweza kuvumilia haya. Na kabla ya misukosuko hii wote walikuwa pamoja — Waislamu wa kweli na wale wanafiki — wala hawawezi kupambanuka. Sasa kwa misukosuko hii wanapambanuka. Na lau kuwa si misukosuko hii wasingepambanuka kwani Mwenyezi Mungu hamjulishi ghaibu yake kiumbe yo yote isipokuwa Mitume.

Wanaojidai wanajua ilimu ya ghaibu (kama hao watazamiaji manazili na wapiga bao) waongo kabisa — hapana ruhusa kuwendea kuwauliza.

180. Mwenyezi Mungu anawahadharisha mabakhili kuwa wasione tamu kwa ubakhili wao huo. Mali zao zitageuzwa majoka yawatatize na kuwasakama shingoni mwao.

181. Mayahudi walikuwa wakifanya stihzai alipokuwa Mtume anawahimiza matajiri kuwatazama mafakiri. Wakasema "Mwenyewe Mwenyezi Mungu amekuwa masikini. Sisi ndio matajiri tunamlishia viumbe Vyake."

Ubaya wao waliofanya huo wa kuua Mitume hauwatoshi. Sasa wanamfanyia stihzai Mungu.

182. Haya ni baadhi ya maneno watakayoambiwa watakapotiwa Motoni.

183. Mayahudi walipokuwa wanaambiwa na Mtume wamfuate, walikuwa wakisema "Sisi hatukuamrishwa kufuata Mitume wanaokubalisha sadaka kuliwa na watu. Tumeamrishwa kuwafuata wale Mitume ambao hukusanya sadaka zote, kisha wakazitia moto (au ukaja moto) ukazila (ukaziunguza) sadaka hizo."

Nao kweli walikuja Mitume namna hao; lakini hawakuwafuata chochote, kama alivyosema hapa Mwenyezi Mungu. Wala hawakuamrishwa kuwa wasiwafuate ila Mitume namna hao tu. Hicho ni kisingizio cha uwongo wanachosingizia.

185. Kila nafsi itaonja mauti. Na bila shaka mtapewa ujira wenu kamili siku ya Kiyama. Na aliyewekwa mbali na moto na akaingizwa Peponi, basi amefuzu (amefaulu kweli kweli). Na maisha ya dunia (hii) si kitu ila ni starehe idanganyayo (watu).

كُلُّ نَفْسٍ ذَآئِقَةُ الْمَوْتِ ۗ وَإِنَّمَا تُوَفَّوْنَ أُجُورَكُمْ يَوْمَ الْقِيٰمَةِ ۖ فَمَنْ زُحْزِحَ عَنِ النَّارِ وَأُدْخِلَ الْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَ ۗ وَمَا الْحَيٰوةُ الدُّنْيَآ إِلَّا مَتٰعُ الْغُرُورِ ﴿١٨٥﴾

186. Mtapata misukosuko katika mali zenu na nafsi zenu, na mtasikia udhia mwingi kwa wale waliopewa Kitabu kabla yenu, na kwa wale walioshirikisha (Waarabu). Na kama mkisubiri na kujilinda na aliyoyakataza Mwenyezi Mungu (mtakuwa mmefanya jambo zuri); kwani mambo haya ni katika mambo makubwa ya kuazimia mtu kuyafanya.

لَتُبْلَوُنَّ فِيٓ أَمْوٰلِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ وَلَتَسْمَعُنَّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتٰبَ مِنْ قَبْلِكُمْ وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُوٓا أَذًى كَثِيرًا ۚ وَإِنْ تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا فَإِنَّ ذٰلِكَ مِنْ عَزْمِ الْأُمُورِ ﴿١٨٦﴾

187. Na (wakumbushe) Mwenyezi Mungu alipofunga ahadi na wale waliopewa Kitabu (akawaambia): "Lazima mtakibainisha kwa watu wala hamtakificha." Lakini walikitupa nyuma ya migongo yao na walikhitari mali chache (ya kidunia kuliko waliyoamrishwa kuyafuata katika Kitabu hicho). Basi ubaya ulioje kwa kukhitari kwao huko.

وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثٰقَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتٰبَ لَتُبَيِّنُنَّهُ لِلنَّاسِ وَلَا تَكْتُمُونَهُ فَنَبَذُوهُ وَرَآءَ ظُهُورِهِمْ وَاشْتَرَوْا بِهِۦ ثَمَنًا قَلِيلًا ۖ فَبِئْسَ مَا يَشْتَرُونَ ﴿١٨٧﴾

188. Usidhani wale wanaofurahia mambo (mabaya) waliyoyafanya, na wakapenda kusifiwa kwa yale wasiyoyafanya; usidhani wao watasalimika na adhabu; (la, bali) itakuwa kwao adhabu iumizayo.

لَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَفْرَحُونَ بِمَآ أَتَوا وَّيُحِبُّونَ أَنْ يُحْمَدُوا بِمَا لَمْ يَفْعَلُوا فَلَا تَحْسَبَنَّهُمْ بِمَفَازَةٍ مِّنَ الْعَذَابِ ۖ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٨٨﴾

189. Na ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.

وَلِلَّهِ مُلْكُ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَاللَّهُ عَلٰى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٨٩﴾

190. Katika kuumbwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana, ziko hoja (za kuonyesha kuwapo Mwenyezi Mungu mmoja), kwa wenye akili

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلٰفِ الَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَأٰيٰتٍ لِّأُولِي الْأَلْبٰبِ ﴿١٩٠﴾

191. Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa na wakilala. Na hufikiri umbo la mbingu na ardhi (pia. 'Namna gani Mwenyezi Mungu alivyoumba'. Wakasema:) "Mola wetu! Hukuviumba hivi bure. Utukufu ni wako. Basi tuepushe na adhabu ya Moto."

الَّذِينَ يَذْكُرُونَ اللَّهَ قِيٰمًا وَقُعُودًا وَعَلٰى جُنُوبِهِمْ وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلْقِ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۚ رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هٰذَا بٰطِلًا ۚ سُبْحٰنَكَ فَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿١٩١﴾

---

185. Wanahimizwa watu wayachume ya kuwatia Peponi na wayaepuke ya kuwatia Motoni, kwani Moto ni natija ya amali zao; na Pepo vile vile.

186. Wanahimizwa Waislamu wasijibizane na wabaya. Na wastahamili waendelee na yao — bila ya kuyawacha — kwani Mstahamlivu Hula Mbivu.

191. Yaani wanaomkumbuka Mwenyezi Mungu kila wakati. Na zimetajwa sifa zao nyingine.

192. "Mola wetu! Wale ambao utawaingiza Motoni, basi itakuwa umewadhalilisha na hawatakuwapo wasaidizi kwa ajili ya madhalimu."

رَبَّنَا إِنَّكَ مَن تُدْخِلِ النَّارَ فَقَدْ أَخْزَيْتَهُ ۖ وَمَا
لِلظَّالِمِينَ مِنْ أَنصَارٍ ﴿١٩٢﴾

193. "Mola wetu! Tumesikia mwitaji anayeita kwendea Uislamu kwamba: 'Mwaminini Mola wenu.' Tukaamini. Mola wetu! Tusamehe madhambi yetu na utufutie (aibu ya) makosa yetu (hayo) na utufishe pamoja na watu wema."

رَبَّنَا إِنَّنَا سَمِعْنَا مُنَادِيًا يُنَادِي لِلْإِيمَانِ أَنْ
آمِنُوا بِرَبِّكُمْ فَآمَنَّا ۚ رَبَّنَا فَاغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا
وَكَفِّرْ عَنَّا سَيِّئَاتِنَا وَتَوَفَّنَا مَعَ الْأَبْرَارِ ﴿١٩٣﴾

194. "Mola wetu! Na utupe uliyotuahidi kwa (ndimi za) mitume yako, wala usitufedheheshe siku ya Kiyama; bila shaka wewe huvunji miadi."

رَبَّنَا وَآتِنَا مَا وَعَدتَّنَا عَلَىٰ رُسُلِكَ وَلَا تُخْزِنَا
يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ إِنَّكَ لَا تُخْلِفُ الْمِيعَادَ ﴿١٩٤﴾

195. Mola wao akawakubalia (maombi yao kwa kusema): "Hakika mimi sitapoteza juhudi (amali) ya mfanya juhudi miongoni mwenu, akiwa mwanamume au mwanamke; (kwani nyinyi) ni nyinyi kwa nyinyi. Basi waliohama (miji yao kwa khiari yao) au kufukuzwa katika miji yao na kuudhiwa katika njia yangu, na wakapigana na kuuawa; kwa yakini nitawafutia makosa yao, na nitawaingiza katika mabustani yanayopita mito mbele yake. Ndiyo malipo yanayotoka kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu kwake kuna malipo mema (kabisa).

فَاسْتَجَابَ لَهُمْ رَبُّهُمْ أَنِّي لَا أُضِيعُ عَمَلَ
عَامِلٍ مِّنكُم مِّن ذَكَرٍ أَوْ أُنثَىٰ ۖ بَعْضُكُم مِّن
بَعْضٍ ۖ فَالَّذِينَ هَاجَرُوا وَأُخْرِجُوا مِن دِيَارِهِمْ
وَأُوذُوا فِي سَبِيلِي وَقَاتَلُوا وَقُتِلُوا لَأُكَفِّرَنَّ
عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَلَأُدْخِلَنَّهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن
تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ثَوَابًا مِّنْ عِندِ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ عِندَهُ
حُسْنُ الثَّوَابِ ﴿١٩٥﴾

196. Kusikudanganye kwenda na kurudi kwa makafiri katika miji.

لَا يَغُرَّنَّكَ تَقَلُّبُ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي الْبِلَادِ ﴿١٩٦﴾

197. Ni starehe ndogo. Kisha makazi yao yatakuwa Jahannam. Na ni mahali pabaya palioje pa kupumzikia (mtu).

مَتَاعٌ قَلِيلٌ ثُمَّ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ ۚ
وَبِئْسَ الْمِهَادُ ﴿١٩٧﴾

198. Lakini waliomcha Mola wao watapata Mabustani (Pepo) yanayopita mito mbele yake. Watakaa humo milele. Ndiyo makaribisho yao yatokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na vilioko kwa Mwenyezi Mungu ni bora kabisa kwa watu wema (kuliko starehe hizi wanazozipata wabaya duniani).

لَٰكِنِ الَّذِينَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ لَهُمْ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِن
تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا نُزُلًا مِّنْ عِندِ
اللَّهِ ۗ وَمَا عِندَ اللَّهِ خَيْرٌ لِّلْأَبْرَارِ ﴿١٩٨﴾

199. Katika watu waliopewa Kitabu wako wanaomwamini Mwenyezi Mungu na

وَإِنَّ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَمَن يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ

---

192. Madhalimu hawatapata wa kuwanusuru huko. Watateswa tu. Basi wanahimizwa wajiepushe na dhulma upesi.

193. Zinatajwa baadhi ya dua zao wanazoziomba mara nyingi.

195. Waislamu wote ni sawa sawa — kitu kimoja. Kama watakavyolipwa wanaume kwa amali zao ndivyo watakavyolipwa wanawake; bila ya hawa kupewa thawabu zaidi wala wale kupewa thawabu kasoro; wakiwa waungwana au watumwa. Wote kwa Mwenyezi Mungu sawa sawa. Na zinatajwa daraja kubwa kabisa wanazozipata wanaotaabika kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu.

196-198. Mtu mwema asivunjike moyo akiona wabaya wanatengenekewa. Aendelee tu na jitihadi yake. Ima atalipwa Akhera au atalipwa na duniani pia. Ama hao, wanalipwa papa hapa duniani tu. Basi asijishughulishe kwa kujihuzunisha; ashughulike kwa kutengeneza yake yaongoke.

yaliyoteremshwa kwenu na yaliyoteremshwa kwao, kwa kumnyenyekea Mwenyezi Mungu. Hawaziuzi Aya za Mwenyezi Mungu kwa thamani ndogo (ya kidunia. Kwa hivyo wamesilimu). Hao wana ujira wao kwa Mola wao. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.

إِلَيْكُمْ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْهِمْ خَٰشِعِينَ لِلَّهِ ۙ لَا يَشْتَرُونَ
بِـَٔايَٰتِ ٱللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا ۗ أُولَٰٓئِكَ لَهُمْ أَجْرُهُمْ عِندَ
رَبِّهِمْ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ سَرِيعُ ٱلْحِسَابِ ﴿١٩٩﴾

200. Enyi mlioamini! Subirini na muwashinde makafiri (katika kusubiri), na kuweni imara (nyoyo zenu) na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kufaulu (kufuzu).

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا ٱصْبِرُوا وَصَابِرُوا وَرَابِطُوا ۟
وَٱتَّقُوا ٱللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٢٠٠﴾

---

200. Haya ndiyo ya kufanywa na yaliyo kama haya. Anayefanya haya atatengenekewa tu. Msitahamilivu hula mbivu; hawi mtovu wala hali mbovu.

Wanaosubiri wakaendelea kufanya taa· (utii) na kujiepusha na mabaya mpaka kufa kwao. Na wakasubiri misiba na misukosuko inayowafika. Wakasimama imara wakatengeneza yao hayo yaliyoharibika. Siyo kufunga mikono na tamaa ikawatamauka. Ukiharibikiwa tazama nini kilichokuharibia. Uanze tena na kujiepusha na hilo lilokuharibia. Au ushike jengine unaloona kuwa litakuwa bora kuliko hilo lililokuharibia. Siyo kushika tama na kulia.

Na vilevile wakawasubiria na kuwastahamilia wanaokaa nao kwa maovu yao na wanaokutana nao kwa mabaya wanayowatendea; wasiwalipe kwa maovu yao. bali wawe wanawasamehe na kuwachukulia. Khasa wazee wao na watoto wao na wake zao (na waume zao) na jamaa zao wengine na watumishi wao na walio kama hawa.

Ukae na watu wote kwa vizuri. Unawastahamilia na unawafanyia mazuri hata wao wasipokufanyia.

اٰيَاتُهَا ١٧٦ (٤) سُوْرَةُ النِّسَآءِ مَدَنِيَّةٌ (٩٢) رُكُوْعَاتُهَا ٢٤

Ina Aya 176

# SURAT AN - NISA

*Imeteremka Madina*

Ina Makara 24

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo pia.

يٰۤاَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوْا رَبَّكُمُ الَّذِىْ خَلَقَكُمْ مِّنْ نَّفْسٍ وَّاحِدَةٍ وَّخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيْرًا وَّنِسَآءً ۚ وَاتَّقُوا اللّٰهَ الَّذِىْ تَسَآءَلُوْنَ بِهٖ وَالْاَرْحَامَ ؕ اِنَّ اللّٰهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيْبًا ①

1. Enyi watu! Mcheni Mola wenu ambaye amekuumbeni katika nafsi (asli) moja. Na akamuumba mkewe katika nafsi ile ile. Na akaeneza wanaume wengi na wanawake kutoka katika wawili hao. Na mcheni Mwenyezi Mungu ambaye kwaye mnaombana. Na (mwatazame) jamaa. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mlinzi juu yenu (anayaona kila mnayoyafanya).

وَاٰتُوا الْيَتٰمٰٓى اَمْوَالَهُمْ وَلَا تَتَبَدَّلُوا الْخَبِيْثَ بِالطَّيِّبِ ۖ وَلَا تَاْكُلُوْۤا اَمْوَالَهُمْ اِلٰٓى اَمْوَالِكُمْ ؕ اِنَّهٗ كَانَ حُوْبًا كَبِيْرًا ②

2. Na wapeni mayatima mali zao. Wala msibadilishe kibaya kwa kizuri. (Yaani msikhitari cha haramu). Wala msile mali zao pamoja na mali zenu. Hakika (yote) hayo ni jukumu kubwa.

وَاِنْ خِفْتُمْ اَلَّا تُقْسِطُوْا فِى الْيَتٰمٰى فَانْكِحُوْا مَا طَابَ لَكُمْ مِّنَ النِّسَآءِ مَثْنٰى وَثُلٰثَ وَرُبٰعَ ۚ فَاِنْ خِفْتُمْ اَلَّا تَعْدِلُوْا فَوَاحِدَةً اَوْ مَا مَلَكَتْ اَيْمَانُكُمْ ؕ ذٰلِكَ اَدْنٰٓى اَلَّا تَعُوْلُوْا ③

3. Na kama mkiogopa kutowafanyia uadilifu mayatima (basi ogopeni vile vile kutowafanyia uadilifu wanawake). Basi oeni mnaowapenda katika wanawake, (maadamu mtawafanyia insafu) Wawili au watatu au wane (tu). Na mkiogopa kuwa hamwezi kufanya uadilifu, basi (oeni) mmoja tu, au (wawekeni masuria) wale ambao mikono yenu ya kiume imewamiliki. Kufanya hivi ndiko kutapelekea kutofanya jeuri.

---

1. Hapa inaonyeshwa kuwa Bibi Hawa kaumbwa katika Udongo ule ule alioumbiwa Nabii Adamu—siyo kaumbwa katika mbavu za Nabii Adamu; kwa hivi kila mwanamume ana ubavu mmoja wa kushoto kasoro kuliko mwanamke! Habari hii hakusema Mtume ingawa inatajwa katika baadhi ya vitabu vya tafsiri.

Hapa inahimizwa kumcha Mwenyezi Mungu—kumhishimu ukafuata amri Zake na ukajiepusha na makatazo Yake; kwani Yeye ndiye aliyekuumba na akakuumbia vyote alivyokuumbia. Bali hata wewe mwenyewe ukitaka kumtia nguvu mwenzio asikuvunje, akufanyie unalomtaka akufanyie, unamwambia 'Nakuomba kwa jina la Mwenyezi Mungu unifanyie . . .' kwa kuona kuwa hataweza kukuvunja maadam umemtaja Mwenyezi Mungu; unaona kuwa atalipa hishima jina la Mwenyezi Mungu; hatalivunja. Basi mbona wewe unalivunja jina la Mwenyezi Mungu? Unaacha aliyokuamrisha, au unafanya aliyokataza. Unawataka watu wafanye usiyoyafanya wewe! Namna gani hivi!

Na inaambiwa hapa kuwa Mwenyezi Mungu analiona kila jambo wanalolitenda waja Wake; hata likiwa dogo vipi na likafichwa vipi.

3. Wanavyuoni wote wa sharia ya Kiislamu wamekongamana kwamba aya hii imeweka mpaka wa idadi ya wake ambao mtu aweza kuoa, na inakataza mtu kuwa na zaidi ya wake wane wakati mmoja. Hadithi za Mtume pia zinatilia nguvu kongamano hilo. Imehadithiwa kuwa Ghailan, mtemi wa Taif, alikuwa na wake tisia aliposilimu. Mtume akamwambia abakishe wane tu na awataliki wote wengine. Kuna na riwaya ya Naufal bin Muawiyah ambaye, aliposilimu naye, aliamrishwa na Mtume kumtaliki mmoja wa wake zake watano.

Pia inapasa kuzingatia kuwa aya hii, ingawa inatoa ruhusa mtu kuoa mke zaidi ya mmoja, ni sharti awafanyie insafu (awagawie haki zao kwa usawa). Kwa hivyo, mtu yoyote anayeitumia vibaya ruhusa hii kwa kuoa mke zaidi

4. Na wapeni wanawake mahari yao, hali ya kuwa ni hadiya (aliyowapa Mungu). (Lakini hao wake zenu) wakikupeni kwa radhi ya nafsi zao kitu katika hayo (mahari) basi kuleni kwa furaha na kunufaika.

وَاٰتُوا النِّسَآءَ صَدُقٰتِهِنَّ نِحْلَةً ۚ فَاِنْ طِبْنَ لَكُمْ عَنْ
شَيْءٍ مِّنْهُ نَفْسًا فَكُلُوْهُ هَنِيْٓـًٔا مَّرِيْٓـًٔا ﴿٤﴾

5. Wala msiwape wapumbavu mali zenu (mali zao mlizonazo) ambazo Mwenyezi Mungu amezijaalia kwa ajili ya maisha yenu (nyote); na wapeni chakula chao humo na wavisheni na waambieni maneno mazuri.

وَلَا تُؤْتُوا السُّفَهَآءَ اَمْوَالَكُمُ الَّتِيْ جَعَلَ اللّٰهُ
لَكُمْ قِيٰمًا وَّارْزُقُوْهُمْ فِيْهَا وَاكْسُوْهُمْ وَقُوْلُوْا
لَهُمْ قَوْلًا مَّعْرُوْفًا ﴿٥﴾

6. Na wajaribuni mayatima (wanapokuwa karibu ya kubaleghe kama wataweza kutumia fedha zao vizuri wakati watakapobaleghe. Wajaribuni kidogo kidogo) mpaka wafike wakati wa kuoa (kubaleghe). Kama mkiwaona wana akili njema, wapeni mali zao. Wala msizile kwa fujo na kwa haraka ya kwamba watakua (wazitake; hebu tuzile upesi). Na mwenye kuwa tajiri basi ajiepushe (na kuchukua ujira katika kuwafanyia kazi zao). Na atakayekuwa mhitaji basi ale kwa namna inayokubaliwa na Sharia. Na mtakapowapa mali zao, basi wawekeeni mashahidi (juu ya kuwa) Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi.

وَابْتَلُوا الْيَتٰمٰى حَتّٰىٓ اِذَا بَلَغُوا النِّكَاحَ ۚ فَاِنْ
اٰنَسْتُمْ مِّنْهُمْ رُشْدًا فَادْفَعُوْٓا اِلَيْهِمْ اَمْوَالَهُمْ ۚ وَلَا
تَاْكُلُوْهَآ اِسْرَافًا وَّبِدَارًا اَنْ يَّكْبَرُوْا ۗ وَمَنْ كَانَ
غَنِيًّا فَلْيَسْتَعْفِفْ ۚ وَمَنْ كَانَ فَقِيْرًا فَلْيَاْكُلْ
بِالْمَعْرُوْفِ ۚ فَاِذَا دَفَعْتُمْ اِلَيْهِمْ اَمْوَالَهُمْ
فَاَشْهِدُوْا عَلَيْهِمْ ۗ وَكَفٰى بِاللّٰهِ حَسِيْبًا ﴿٦﴾

---

ya mmoja bila ya kufanya insafu, atakuwa anajaribu kumhadaa Mwenyezi Mungu. Kwa sababu hii, mahakama ya nchi za Kiislamu yamepewa uwezo wa kulazimisha kufanywa insafu ili kurakibisha kosa alilofanyiwa mke au wake. Pamoja na hayo, ni kosa kabisa kuchukulia kwamba, kwa kuweka sharti hiyo ya insafu, aya hii imekusudia kuondoa ruhusa ya kuoa wake wengi. Hivyo sivyo inavyosema Qurani; wanaosema hivyo ni wale Waislamu ambao wametekwa akili zao na Wakristo wa nchi za Magharibi. Wao husema kwamba Qurani pia inapinga kuoa wake wengi, lakini haikuliondoa jambo hilo moja kwa moja kwa sababu haikuona kuwa ni jambo la busara kufanya hivyo wakati huo kwa vile ambavyo dasturi yenyewe ilikuwa imeenea. Badala yake, inamruhusu mtu kuoa wake wengi maadamu atawafanyia insafu. Kwa kuwa sharti hii ni ngumu mno kuitekeleza, pendekezo hapa ni kuoa mke mmoja; Kwa hakika, fikira hizo husababishwa na kutawaliwa akili, kwa sababu kuoa wake wengi koo kwenyewe si jambo ovu, kwani wakati mwingine huwa ni jambo la lazima ili kumzuia mja asiipindukie mipaka ya Mwenyezi Mungu. Kuna watu wengine, hata wakitaka, hawatosheki na mke mmoja. Ruhusa ya kuoa wake mpaka wane huwaepusha watu kama hao na madhara ya uhasharati usio na kifani. Ndio Qurani ikawaruhusu watu kama hao kuoa mpaka wake wane maadamu watawafanyia insafu.

Ama wale wanaoona kuwa ni ufisadi kuoa wake wawili mpaka wane, ni khiari yao kuipinga Qurani na kuibeza ruhusa hiyo, lakini hawana haki ya kuisingizia upotofu wa mawazo yao, maana Qurani imehalalisha jambo hili kwa lugha iliyo wazi bila ya kutumia neno lolote liwezalo kupinduliwa kwa namna yoyote ili liwe na maana kwamba Qurani imekusudia kukataza jambo hili.

4. Kumdai wewe mwanamke mahari yako uliyompa–au kumtoza fedha nyingine–ndiyo huna ruhusa. Lakini mwenyewe—katika furaha zenu–akikutunukia kitu kukupa kipokee: usimkatalie utamvunja. Kama wewe unavyompa na yeye anaweza kukupa.

5. Mawasii—kama walivyoambiwa—wasiwadhulumu mayatima, wawape haki yao kamili ndivyo wanavyoambiwa hapa vile vile kuwa waendelee kuwatazamia mali zao hao mayatima wala wasiwape wenyewe maadamu bado wapumbavu, wabadhirifu, hawajui kima cha mali, wanatumia ovyo ovyo. Basi wasiwape wenyewe japo wamekwisha baleghe. Waendelee kuendesha na kuwaambia maneno mazuri kama vile kuwaambia 'Bado nakuona si hodari wa kudhibiti chako. Utakitosa bure. Wacha nikuendeshee tu vivi hivi mpaka siku za mbele kidogo. Nikikuona imetua makini yako, unaweza kujimiliki katika tasarufu zako nitakupa mwenyewe.' Na kama hivi.

Kwani hayo mali ya huyo yatima yakipotezwa kwa njia za batili hatakuwa huyo yatima tu ndiye aliyekosa; bali njia za kheri zitakuwa zimekosa. Mali ndicho kitengezaji kikubwa cha kila kheri.

7. Wanaume wana sehemu katika mali wanayoyaacha wazazi na jamaa waliokaribia. Na wanawake (pia) wanayo sehemu katika yale waliyoyaacha wazazi na jamaa waliokaribia. Yakiwa kidogo au mengi. (Hivi) ni sehemu zilizofaridhiwa (na Mwenyezi Mungu).

لِلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ الْوَالِدٰنِ
وَالْأَقْرَبُونَ ۖ وَلِلنِّسَاءِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ
الْوَالِدٰنِ وَالْأَقْرَبُونَ مِمَّا قَلَّ مِنْهُ أَوْ كَثُرَ ۚ
نَصِيبًا مَّفْرُوضًا ﴿٧﴾

8. Na wakati wa kugawanya wakihudhuria jamaa na mayatima na masikini, wapeni kitu katika hayo (mali ya urithi) na waambieni kauli njema.

وَإِذَا حَضَرَ الْقِسْمَةَ أُولُوا الْقُرْبٰى وَالْيَتٰمٰى
وَالْمَسٰكِينُ فَارْزُقُوهُم مِّنْهُ وَقُولُوا لَهُمْ قَوْلًا
مَّعْرُوفًا ﴿٨﴾

9. Na waogope (mawasii kuwadhulumu mayatima; na wakumbuke) kama na wao wangewacha nyuma yao watoto madhaifu wangekuwa na khofu juu yao; basi wamwogope Mwenyezi Mungu na waseme maneno yaliyo sawa (kwa hao mayatima waliousiwa kuwatazama).

وَلْيَخْشَ الَّذِينَ لَوْ تَرَكُوا مِنْ خَلْفِهِمْ ذُرِّيَّةً ضِعٰفًا
خَافُوا عَلَيْهِمْ ۖ فَلْيَتَّقُوا اللّٰهَ وَلْيَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا ﴿٩﴾

10. Hakika wale ambao wanakula mali ya mayatima kwa dhuluma, bila shaka wanakula moto matumboni mwao; na wataungua katika huo Moto (wa Jahannam) uwakao.

إِنَّ الَّذِينَ يَأْكُلُونَ أَمْوٰلَ الْيَتٰمٰى ظُلْمًا إِنَّمَا
يَأْكُلُونَ فِي بُطُونِهِمْ نَارًا ۖ وَسَيَصْلَوْنَ سَعِيرًا ﴿١٠﴾

11. Mwenyezi Mungu anakuusieni juu ya watoto wenu; mwanamume apate sawa na sehemu ya wanawake wawili. Na ikiwa wanawake ni (wawili au) zaidi ya wawili, basi watapata thuluthi mbili za (mali) aliyoiacha (maiti). Lakini akiwa mtoto mwanamke ni mmoja, basi apewe nusu. Na wazazi wake wawili, kila mmoja wao apate sudusi (sehemu ya sita) ya (mali) aliyoiacha (maiti), akiwa (maiti huyo) anaye mtoto (au mjukuu). Lakini kama hana mtoto, na wazazi wake wawili wamekuwa ndio warithi wake, basi mama yake atapata thuluthi moja (na baba

يُوصِيكُمُ اللّٰهُ فِي أَوْلٰدِكُمْ ۖ لِلذَّكَرِ مِثْلُ حَظِّ
الْأُنثَيَيْنِ ۚ فَإِن كُنَّ نِسَاءً فَوْقَ اثْنَتَيْنِ فَلَهُنَّ
ثُلُثَا مَا تَرَكَ ۖ وَإِن كَانَتْ وٰحِدَةً فَلَهَا النِّصْفُ ۚ
وَلِأَبَوَيْهِ لِكُلِّ وٰحِدٍ مِّنْهُمَا السُّدُسُ مِمَّا تَرَكَ
إِن كَانَ لَهُ وَلَدٌ ۚ فَإِن لَّمْ يَكُن لَّهُ وَلَدٌ وَوَرِثَهُ
أَبَوَاهُ فَلِأُمِّهِ الثُّلُثُ ۚ فَإِن كَانَ لَهُ إِخْوَةٌ فَلِأُمِّهِ
السُّدُسُ مِن بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصِي بِهَا أَوْ دَيْنٍ

6. Lakini inataka awe akimjaribujaribu katika kumwachia kutasarafu kidogo kidogo kila mara ili achume ujuzi wa kutumia, awe hodari kama walivyo hao mahodari. Akishamwona kafikilia daraja hiyo ampe mwenyewe—asijidai kutoa udhuru huu na huu wa uwongo ili ziselehee kukaa kwake daima, au zikae zaidi kuliko inavyotakikana. Asifanye hivyo.

7. Hapa inaingiwa kutaja habari za kurithi: Kuwa kwa Kiislamu wanawake wanawarithi jamaa zao—sio kuwa wanaume tu ndio wanaorithi.

Lakini sehemu anayopewa mwanamke huwa ni ndogo kuliko sehemu anayopewa mwanamume, kwani mwanamume ndiye mwenye mas-ulia (responsibilities) mengi kuliko mwanamke. Mwanamume ana mas-ulia ya kumtazama mkewe, wanawe na wazee. Ama mwanamke hana màs-ulia katu juu ya mumewe, wala hana mas-ulia juu ya wanawe mpaka baba awe hohe hahe hana mbele hana nyuma, wala kufanya kazi hakumudu — na huyo mama ana hali nzuri. Hapo ndipo itapompasa mama kutazama wanawe.

Na mas-ulia yake mwanamke ya kutazama wazee wake ni nusu ya mas-ulia ya ndugu yake, (mwanamume).

8. Mali ni kitu kinachotokewa roho na wanadamu wote khasa kikionekana kana kwamba kinapatikana bure—kama mali ya kurithi. Basi wale wasiopata hufanya kijicho sana. Ndiyo maana akasema hapa Mwenyezi Mungu kwamba katika kugawanywa hayo mali ya urithi wakitokea jamaa hivi wapewe kitu kidogo na watakwe radhi kwa kuwa hicho wanachopewa ni kidogo.

9. Wanakumbushwa mawasii kuwa wasione tamu kuwadhili watoto wa watu. Wajikumbuke kuwa na wao mara moja wanaweza kufa wakaacha watoto wao nyuma, wakadhiliwa kama wanavyowadhili wa watu. 'Mla cha

thuluthi mbili). Na kama (huyo maiti) anao ndugu, basi mama yake atapata sudusi (sehemu ya sita). Na huku kurithi kunakuwa) baada ya kutoa aliyoyausia au kulipa deni. Baba zenu na watoto wenu: nyinyi hamjui ni nani miongoni mwao aliye karibu zaidi kukunufaisheni. (Hiyo) ni Sharia iliyotoka kwa Mwenyezi Mungu. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mjuzi(na)Mwenye hikima.

ءَابَآؤُكُمْ وَأَبْنَآؤُكُمْ لَا تَدْرُونَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ لَكُمْ
نَفْعًا ۚ فَرِيضَةً مِّنَ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا
حَكِيمًا ⑪

12. Na nyinyi mtapata nusu ya (mali) walizoacha wake zenu, kama wao hawana mtoto (wala mjukuu). Na ikiwa wana mtoto (au mjukuu), nyinyi mtapata robo ya walivyoacha. Baada ya kutoa walivyousia au kulipa deni. Nao (wake zenu) watapata robo ya mlivyoacha, ikiwa hamna mtoto, (wala mjukuu). Lakini ikiwa mnaye mtoto (au mjukuu), basi wao (hao wanawake) watapata thumni (sehemu ya nane) ya vile mlivyoacha. Baada ya kutoa mlivyousia au kulipa deni. Na kama mwanamume au mwanamke anayerithiwa hana mtoto (wala mjukuu) wala wazazi, lakini anaye kaka (wa kwa mama) au dada (wa kwa mama pia), basi kila mmoja katika hawa atapata sudusi (sehemu ya sita). Na wakiwa zaidi kuliko hivyo basi watashirikiana katika thuluthi (sehemu ya tatu). Baada ya kutoa vilivyousiwa au kulipa deni, pasipo kuleta dhara. (Huu) ndio wasia uliotoka kwa Mwenyezi Mungu. na Mwenyezi Mungu Ni Mjuzi (na) Mwenye Upole.

وَلَكُمْ نِصْفُ مَا تَرَكَ أَزْوَاجُكُمْ إِن لَّمْ يَكُن لَّهُنَّ
وَلَدٌ ۚ فَإِن كَانَ لَهُنَّ وَلَدٌ فَلَكُمُ الرُّبُعُ مِمَّا
تَرَكْنَ ۚ مِنۢ بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصِينَ بِهَآ أَوْ دَيْنٍ ۚ
وَلَهُنَّ الرُّبُعُ مِمَّا تَرَكْتُمْ إِن لَّمْ يَكُن لَّكُمْ وَلَدٌ ۚ
فَإِن كَانَ لَكُمْ وَلَدٌ فَلَهُنَّ الثُّمُنُ مِمَّا
تَرَكْتُم ۚ مِّنۢ بَعْدِ وَصِيَّةٍ تُوصُونَ بِهَآ أَوْ دَيْنٍ ۗ وَ
إِن كَانَ رَجُلٌ يُورَثُ كَلَٰلَةً أَوِ امْرَأَةٌ وَلَهُۥٓ أَخٌ
أَوْ أُخْتٌ فَلِكُلِّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا السُّدُسُ ۚ فَإِن كَانُوٓا
أَكْثَرَ مِن ذَٰلِكَ فَهُمْ شُرَكَآءُ فِى الثُّلُثِ ۚ مِنۢ بَعْدِ
وَصِيَّةٍ يُوصَىٰ بِهَآ أَوْ دَيْنٍ غَيْرَ مُضَآرٍّ ۚ وَصِيَّةً
مِّنَ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَلِيمٌ ⑫

---

mwenziwe na chake huliwa.'

11. Hapa inapambanuliwa namna ya urithi kwamba:– (a) Akifa mtu akaacha watoto wanaume na wanawake, basi kila mwanamume atapata mara mbili kuliko kila mwanamke (b) Akifa akaacha watoto wanawake tu—wawili au zaidi kuliko wawili (wala hakuacha mtoto mwanamume hata mmoja)– basi watoto hao watachukua thuluthi mbili za mali, wagawanye wote sawa; pasi na mmoja kumzidi mwenziwe. Na thuluthi iliyozidi itarithiwa na mawarithi wengine kama wako. Kama hapana watarejeshewa wenyewe wale watoto wanawake.

*N.B.* Thuluthi mbili ni kugawa yale mali sehemu tatu sawa sawa, na hao wakachukua sehemu mbili katika tatu hizo. Na (c) Akifa akaacha mtoto mwanamke mmoja tu (wala hana ndugu mwanamume), basi mali yatagawiwa sehemu mbili. Sehemu moja (yaani nusu yake) atapewa huyu mtoto. Na nusu iliyosalia watapewa warithi wengine kama wapo. Kama hapana atarejeshewa mwenyewe huyo mtoto mwanamke.

Hukumu ya wajukuu ni kama hukumu ya watoto inapokuwa maiti huyo hana mtoto — ana wajukuu.

Na (d) Akifa mtu akaacha watoto wake (au wajukuu wake) na wazee wake (baba na mama), basi baba atapata sudusi yake na mama atapata sudusi yake. Na mali yaliyosalia warithi wale watoto wa maiti au wajukuu.

Na sudusi ni mali ile kugawiwa sehemu 6 na yeye akachukua sehemu moja. Na (e) Akifa mtu akamwacha baba yake na mama yake tu pasina watoto wala wajukuu; basi mama atachukua thuluthi moja ya mali; na thuluthi mbili atazichukua baba. Na (f) Akifa mtu akamwacha mama tu na ndugu zake—wakiwa makhalisa, au kuumeni (kiumeni) au wa kukeni (kiukeni) au wanaume au wanawake au mchanganyiko—mama atachukua sudusi ya mali.

Mawarithi hawana ruhusa kurithi mpaka zilipwe (a) Deni zote za huyo maiti anazodaiwa. Na zitolewe (b) Nyasia alizousia. Wasiwe warithi wepesi kupapia mali ya kurithi. Sharti yatolewe haya kwanza. Lakini huo wasia sharti usiwe wa kuwadhuru hao mawarithi wake, kama ilivyotajwa katika Aya ya 12. Hana ruhusa kuusia zaidi ya thuluthi ya mali yake.

13. Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na anayemtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, (Mwenyezi Mungu) atamwingiza katika Bustani zipitazo mito mbele yake; wakae humo milele. Na huko ndiko kufaulu kukubwa.

تلك حدود الله ، ومن يطع الله ورسوله يدخله
جنت تجري من تحتها الانهر خلدين فيها ،
وذلك الفوز العظيم ﴿١٣﴾

14. Na anayemwasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na kuiruka mipaka yake, (Mwenyezi Mungu) atamwingiza Motoni, humo atakaa milele, na atapata adhabu zifedheheshazo.

ومن يعص الله ورسوله ويتعد حدوده
يدخله نارا خالدا فيها ، وله عذاب مهين ﴿١٤﴾

15. Na wale wanawake wafanyao machafu (ya wenyewe kwa wenyewe) miongoni mwa wanawake wenu; basi washuhudishieni mashahidi wane (waliowaona wanafanya hivyo) miongoni mwenu. Na kama wakishuhudia, basi wazuieni majumbani mpaka mauti yawafishe au Mwenyezi Mungu awafanyie njia nyengine (kama kupata waume kuwaoa, na kama haya).

والتي يأتين الفاحشة من نسائكم فاستشهدوا
عليهن اربعة منكم ، فان شهدوا فامسكوهن
في البيوت حتى يتوفىهن الموت او يجعل الله
لهن سبيلا ﴿١٥﴾

16. Na wale wanaume wawili wanaofanya uchafu (wa wanaume kwa wanaume) miongoni mwenu, waadhibuni wote wawili. Na wakitubia na wakatengenea waacheni. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye apokeaye toba (na) ndiye Mwenye kurehemu.

والذان يأتينها منكم فاذوهما ، فان تابا
واصلحا فاعرضوا عنهما ، ان الله كان
توابا رحيما ﴿١٦﴾

17. Toba inayopokelewa na Mwenyezi Mungu ni ya wale wanaofanya uovu kwa ujinga, kisha wakatubia kwa upesi. Hao ndio Mwenyezi Mungu huipokea toba yao. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima.

انما التوبة على الله للذين يعملون السوء
بجهالة ثم يتوبون من قريب فاولئك يتوب
الله عليهم ، وكان الله عليما حكيما ﴿١٧﴾

---

12. Hapa unatajwa urithi wa watu wengine kuwa :— (a) Akifa mke akamwacha mume (wala hakuacha mtoto wala mjukuu, la mwanamume wala mwanamke) basi mume atapata nusu ya mali aliyoyaacha huyo mkewe. Na (b) Akifa mke akamwacha mume na mtoto (au mjukuu), basi mume atapata robo ya mali.

Na Robo ni kugaiwa sehemu nne akachukua sehemu moja. Na (c) Akifa mume akamwacha mke (bila kuacha mtoto wala mjukuu), basi mke atapata robo ya mali ya mumewe. Na yaliyosalia yarithiwe na mawarithi wengine. Na (d) Akifa mume akamwacha mke na mtoto au mjukuu, basi mke atapata thumni ya mali ya mume.

Na thumni ni kugaiwa sehemu nane akachukua sehemu moja. Na (e) Akifa mtu asiwache mtoto (wala mjukuu) wala wazee; lakini kaacha ndugu mmoja tu wa kwa mama (mwanamume au mwanamke), basi ndugu huyo atapata sudusi ya mali. Na kilichosalia warithi mawarithi wengine. Ikiwa hapana mawarithi wengine atarejeshewa huyu ndugu. Na (f) Akifa mtu asiache mtoto (wala mjukuu) wala wazazi; lakini kaacha ndugu wa kwa mama—wawili au zaidi, wanaume au wanawake au mchanganyiko—ndugu hawa watachukua thuluthi ya mali ya maiti, pasina mwanamume kumzidi mwanamke wala mwanamke kupunguka kuliko mwanamume.

15 – 16. Hizi ni Aya zinazotaja adabu ya kutiwa (a) wanawake wanaofanyana machafu na (b) wanaume wanaofanyana machafu, na (c) wanawake wanaofanya machafu na wanaume. yote haya mabaya kabisa; na zaidi ni yale ya wanaume kwa wanaume, kisha ya wanaume na wanawake, na baadaye wanawake kwa wanawake.

17. Ni kuonyesha kuwa Mwenyezi Mungu anakubali toba ya kila mwenye kutubia; lakini kwa hizi sharti mbili alizozitaja katika Aya hii (a) Kutubia upesi—sio umekwishakuwa mgonjwa, uko kitandani, ndio unasema kuwa 'Sasa natubia' (b) Kuwa kalifanya jambo lile kwa ujinga (yaani yale matamanio yamemvaa saa ile hata yamemtia ujingani kama kwamba hajui adhabu kubwa inayomngojea. Sio kuwa jambo lile la maasi analifanya kila

18. Hawana toba wale ambao hufanya maovu mpaka mauti yamemhudhuria mmoja wao, (hapo) akasema: "Hakika mimi sasa natubu." Wala (hawana toba) wale ambao wanakufa katika hali ya ukafiri. Hao tumewaandalia adhabu iumizayo.

وَلَيْسَتِ التَّوْبَةُ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ ۚ حَتَّىٰ إِذَا
حَضَرَ أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ إِنِّي تُبْتُ الْآنَ وَلَا
الَّذِينَ يَمُوتُونَ وَهُمْ كُفَّارٌ ۚ أُولَٰئِكَ أَعْتَدْنَا لَهُمْ
عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٨﴾

19. Enyi mlioamini! Si halali kwenu kurithi wanawake kwa jeuri. Wala msiwazuie (kuolewa na waume wengine kwa kuwa hamuwataki wala hamtaki kuwaacha ila kwa pesa) ili mpate kuwanyang'anya baadhi ya vile mlivyowapa. (Hapana ruhusa haya) isipokuwa wawe wamefanya uovu ulio wazi. Na kaeni nao kwa wema; na kama mkiwachukia basi (msiwaache) kwani huwenda mkakichukia kitu, na Mwenyezi Mungu ametia kheri nyingi ndani yake.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا يَحِلُّ لَكُمْ أَنْ تَرِثُوا
النِّسَاءَ كَرْهًا ۖ وَلَا تَعْضُلُوهُنَّ لِتَذْهَبُوا
بِبَعْضِ مَا آتَيْتُمُوهُنَّ إِلَّا أَنْ يَأْتِينَ بِفَاحِشَةٍ
مُبَيِّنَةٍ ۚ وَعَاشِرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۚ فَإِنْ
كَرِهْتُمُوهُنَّ فَعَسَىٰ أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَيَجْعَلَ
اللَّهُ فِيهِ خَيْرًا كَثِيرًا ﴿١٩﴾

20. Na kama mkitaka kubadilisha mke mahali pa mke, (yaani kumwoa mke mwengine na kumwacha huyo wa zamani), na hali mmoja wao (naye ndiye huyo unayemwacha) mmempa mrundi wa mali, basi msichukue cho chote. Je, mnachukua kwa dhulma na kwa khatia iliyo wazi?

وَإِنْ أَرَدْتُمُ اسْتِبْدَالَ زَوْجٍ مَكَانَ زَوْجٍ وَآتَيْتُمْ
إِحْدَاهُنَّ قِنْطَارًا فَلَا تَأْخُذُوا مِنْهُ شَيْئًا ۚ
أَتَأْخُذُونَهُ بُهْتَانًا وَإِثْمًا مُبِينًا ﴿٢٠﴾

---

siku—bila ya kujali wala kubali hata kidogo—kama kwamba ni jambo la dasturi linalofanywa daima. Huyu ni jeuri, hajali, basi huyu Mwenyezi Mungu atamuadhibu. Inataka anayeasi awe anaogopa, anajiona kuwa mbaya, anakosa; sio kuwa habali hajali, kama hao walao riba au kudhulumu mayatima na wengineo katika hayo majumba ya kurithisha. Kila usiku uchao wanazidi kuyaonea tamu hayo wanayoyafanya; hao hawana dalili ya kusalimika na Moto.

19. Hapo katika zama za kabla ya Uislamu ilikuwa hivi:– Akifa baba mtu, wanawe wanarithi wake waliokuwa wa baba yao—wasiowazaa wao. Kila mtu atamrithi yule asiyemzaa yeye. Kisha, Wakitaka (a) Watawaoa au (b) Watawaoza waume wawatakao wao (na wapokee wao mahari, wayale) au (c) Watawadhili na kuwataabisha mwisho wa kuwataabisha mpaka wajikomboe kwa fedha watakazo wao (d) Au wadumu vivyo hivyo katika kifungo hicho mpaka wafe.

Basi wanakatazwa hapa kufanya hayo; jeuri hizo za Kijahili zimekwishakwisha.

Na walikuwa wanaume wengine vile vile wanaowadhili na kuwataabisha wake zao wenyewe—wanapoazimia kuwaacha—ili wachoke wajikomboe kwa fedha walizowaolea au kwa vinginevyo. Namna hivi wakifanya makafiri hapo zamani; wakakatazwa na Uislamu.

Lakini kuna wanaojiita Waislamu na wanafanya haya mpaka leo! Basi Waislamu hao? Waislamu kweli! Wapi! Uislamu mchezo wanadhani? Uislamu ni kufuata amri za Mwenyezi Mungu na Mtumewe na kujizuilia na makatazo yao. Jina wala kanzu sio Uislamu. Uislamu ni Nia njema na Maneno latifu na Vitendo vizuri.

Mwanamke humtaki mwache, ende zake akaolewe na atakayemtaka. Huna ruhusa kukaa naye vivyo hivyo tu kwa inda, wala huna ruhusa kumtoza fedha. Ukiweza kukaa naye kwa vizuri—japo humpendi—bora kaa naye.

Ila akiwa yeye mwanamke ndiye mleta uovu na vitendo vibaya vibaya kwa kuwa hakutaki tu wala huna lo lote baya ulilomfanya. Hakutaki tu ndio anakufanyia mizingili mwanambiji hiyo. Basi hapo ndipo unapoweza kumwambia kuwa akikupa mahari yake uliyompa utamwacha. Wala usimtake zaidi kuliko ulivyompa. Wala usikatae kumwacha ukawa unamfanyia inda kuwa "Na mimi sikuachi." Imekatazwa hivi.

Na wahimizwa watu hapa wakae na wake zao kwa vizuri sana; wala wasiwawache hata wakiwa hawawapendi kwani 'Huwenda mkakichukia kitu, na Mwenyezi Mungu ametia kheri nyingi ndani yake'.

Mambo ya kuacha yamechukizishwa sana katika Uislamu. Wanahimizwa watu kuoa na wanavunjwa nguvu kuacha; kinyume cha wanavyofanya Waislamu wengine — Kuoa na Kuacha tu ndiyo kazi yao. Sivyo hivyo.

21. Na mtachukuaje, na hali nyinyi kwa nyinyi mmeingiliana? Nao (wanawake) wamepokea kwenu ahadi thabiti (kuwa mtakaa nao kwa uzuri).

22. Wala msiwaoe wake waliowaoa baba zenu; isipokuwa yale yaliyokwisha pita. (Yaliyopita yamepita yasirejeshwe tena). Bila shaka jambo hili ni uovu na uchukizo na ni njia mbaya.

23. Mmeharimishwa (kuoa) mama zenu, na watoto wenu, na dada zenu, na shangazi zenu, na ndugu za mama zenu, na watoto wa ndugu zenu, na watoto wa dada zenu, na mama zenu waliokunyonyesheni, na dada zenu wa kunyonya, na mama wa wake zenu, na watoto wenu wa kambo walio katika ulinzi wenu, waliozaliwa na wake zenu mliowaingilia. Lakini kama nyinyi hamjawaingilia, basi si vibaya kwenu (kuwaoa). Na (mmeharimishiwa) wake wa watoto wenu waliotoka katika migongo yenu. Na (mmeharimishiwa) kuwaoa

وَكَيْفَ تَأْخُذُونَهُ وَقَدْ أَفْضَىٰ بَعْضُكُمْ إِلَىٰ
بَعْضٍ وَأَخَذْنَ مِنكُم مِّيثَاقًا غَلِيظًا ﴿٢١﴾
وَلَا تَنكِحُوا مَا نَكَحَ آبَاؤُكُم مِّنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَا
قَدْ سَلَفَ ۚ إِنَّهُ كَانَ فَاحِشَةً وَمَقْتًا ۖ
وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٢٢﴾
حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أُمَّهَاتُكُمْ وَبَنَاتُكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ وَ
عَمَّاتُكُمْ وَخَالَاتُكُمْ وَبَنَاتُ الْأَخِ وَبَنَاتُ الْأُخْتِ وَ
أُمَّهَاتُكُمُ اللَّاتِي أَرْضَعْنَكُمْ وَأَخَوَاتُكُم مِّنَ الرَّضَاعَةِ
وَأُمَّهَاتُ نِسَائِكُمْ وَرَبَائِبُكُمُ اللَّاتِي فِي حُجُورِكُم
مِّن نِّسَائِكُمُ اللَّاتِي دَخَلْتُم بِهِنَّ فَإِن لَّمْ تَكُونُوا
دَخَلْتُم بِهِنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ وَحَلَائِلُ أَبْنَائِكُمُ

---

20. Wamepachika uwongo katika hii Aya waliyoifanya kuwa ni ya 21. Wakasema "Sio muradi wa Aya hii kuwa mtu anayo ruhusa ya kumwacha mkewe bure. Lazima pawe na sababu za kutosha." Uwongo! Hapana habari hii. Hapana shaka jambo la kuachana linachukiza katika dini ya Uislamu, na Mtume kasema: "Halali anayoichukia Mwenyezi Mungu ni talaka." Lakini haikuwekwa katika Sharia kuwa "HAISIHI talaka bure bure, lazima pawe na sababu ya kutosha."

20–21. Aya hizi ndizo katika hizo zinazokataza kutoza wake fedha au kuwasamehesha mahari wakati wa kuwawacha. Na watu wakaonea tamu kazi hiyo. Basi itawatia Motoni. Mambo ya kudhulumiana yanamwudhi sana sana Mwenyezi Mungu.

22. Aya hii na zifuatazo zinataja wanawake ambao Sharia imekataza kuwaoa (haramu kuwaoa): (1) Mwanamke aliyepata kuolewa na baba yako, (babu yako, babu wa baba yako—wa kuumeni na kukeni).

Si mke wa ami wala mjomba. Walioachwa na ami au mjomba unaweza kuwaoa. Na walioachwa na ndugu zake babu. (2) Mama aliyekuzaa, (bibi aliyezaa waliokuzaa . . .).(3). Binti wako uliyemzaa (au binti aliyezaliwa na uliyemzaa wewe. . .). (4) Dada yako khalisa au baba mmoja nawe au mama mmoja nawe. (5) Shangazi lako. Ndugu wa baba yako (na ndugu wa babu yako. . .). (6) Mama mdogo. Ndugu wa mama yako (au ndugu wa bibi yako . . .). (7) Binti wa ndugu yako mwanamume, khalisa au wa kwa baba au kwa mama (na kila kilichozaliwa na yeye). (8) Binti wa ndugu yako mwanamke, khalisa au kwa baba au kwa mama (na kilichozaliwa naye). (9) Mama wa kukunyonyesha (na mama zake wa kumzaa au wa kumnyonyesha). (10) Dada yako wa kunyonya naye (aliyenyonyeshwa na aliyekunyonyesha). (11) Mama yake mkeo wa kumzaa au wa kumnyonyesha (na bibi yake pia wa kumzaa na wa kumnyonyesha. . .).

Ama ndugu yake mama yake mkeo (wa kumzaa au kumnyonyesha) unaweza kumwoa akifa huyo mtoto wa nduguye uliye naye au ukimuacha na eda ikesha.

(12) Binti wa mkeo uliyeingia nyumbani naye (na mjukuu wake . . .). Binti wa kumzaa au wa kumnyonyesha na kizazi chake; wote haramu kwako.

Ama ikiwa hukuingia nyumbani naye—akafa au ukamwacha—unaweza kumwoa huyo mwanawe au mjukuu wake . . .

(13) Mke aliyeolewa na mwanao (au mjukuu wako . . .) wa kumzaa mwenyewe (au wa kunyonyeshwa na mkeo); si mtoto wako wa kupanga wala wa kambo. Walioachwa na hao watoto wa kupanga na wa kambo si haramu kwako kuwaoa. (14) Mtu na ndugu yake pamoja (au mtu na shangazi lake au mtu na mama yake mdogo).

Akifa mmoja — au ukimwacha na eda ikisha — unaweza kumwoa wa pili. Lakini kuwa nao wote pamoja (ndugu na nduguye . . .) ndiyo hapana ruhusa.

(15) Mke wa mtu; bado mwenyewe hajafa wala hakumwacha.

Ila wakiwa makafiri na akatekwa huyo mke katika vita vya Jihadi; basi inabatilika ndoa yake. Na baada ya miezi mitatu anaweza kuolewa japo huyo mumewe hajafa wala hakumwacha; na akiwa hana mimba.

madada wawili wakati mmoja; isipokuwa yale yaliyokwishapita. (Yaliyopita yamepita yasirejeshwe tena). Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kurehemu(na) Mwenye kusamehe

الَّذِينَ مِنْ أَصْلَابِكُمْ وَأَنْ تَجْمَعُوا بَيْنَ الْأُخْتَيْنِ
إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٢٣﴾



24. Na pia (mmeharimishiwa) wanawake wenye (waume zao) isipokuwa wale iliyowamiliki mikono yenu ya kuume. (Ndiyo) Sharia ya Mwenyezi Mungu juu yenu. Na mmehalalishiwa (kuoa wanawake) minghairi ya hawa. Muwatafute kwa mali zenu, kwa kuwaoa bila ya kufanya zina. Basi wale mnaowaoa miongoni mwao wapeni mahari yao yaliyolazimishwa. Wala si vibaya kwenu katika (kutoa) yale mliyoridhiana badala ya yale yaliyotajwa. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima.

وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ۖ
كِتَابَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ ۚ وَأُحِلَّ لَكُمْ مَا وَرَاءَ ذَٰلِكُمْ
أَنْ تَبْتَغُوا بِأَمْوَالِكُمْ مُحْصِنِينَ غَيْرَ مُسَافِحِينَ ۚ
فَمَا اسْتَمْتَعْتُمْ بِهِ مِنْهُنَّ فَآتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ
فَرِيضَةً ۚ وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا تَرَاضَيْتُمْ بِهِ
مِنْ بَعْدِ الْفَرِيضَةِ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٢٤﴾

25. Na asiyeweza katika nyiye kupata mali ya kuoa wanawake waungwana Waislamu, (na aoe) katika wajakazi walio Waislamu iliyowamiliki mikono yenu ya kuume (ya kulia). Na Mwenyezi Mungu anajua sana imani yenu; nyinyi kwa nyinyi. (Watumwa na waungwana ni sawa sawa katika Uislamu). Basi waoeni kwa idhini ya mabwana wao na wapeni mahari yao kwa Sharia. (Waoeni na hali ya kuwa) ni wanawake wema wasiokuwa wenye

وَمَنْ لَمْ يَسْتَطِعْ مِنْكُمْ طَوْلًا أَنْ يَنْكِحَ الْمُحْصَنَاتِ
الْمُؤْمِنَاتِ فَمِنْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ مِنْ فَتَيَاتِكُمُ
الْمُؤْمِنَاتِ ۚ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِإِيمَانِكُمْ ۚ بَعْضُكُمْ مِنْ
بَعْضٍ ۚ فَانْكِحُوهُنَّ بِإِذْنِ أَهْلِهِنَّ وَآتُوهُنَّ

---

24. Hapa inabainishwa kuwa kila wanawake wasiokuwa wale waliotajwa ni halali kuwaoa. Na inatajwa kuwa lazima umpe mwanamke mahari yake yaliyotajwa wakati wa kuozwa. Lakini anasema vile vile Mwenyezi Mungu hapa kuwa mwenyewe mwanamke akikubali baadaye kumpunguzia mumewe yale mahari yaliyotajwa, basi khiari yake. Na mume akitaka kumwongezea yule mkewe zaidi kuliko mahari yaliyotajwa, pia khiari yake. Hayo mahari si bei ya mwanamke lakini ni zawadi tu—tunza—anayompa mkewe kuonyesha mahaba yake juu yake. Basi vipi siku ya kumwacha ukamwambia 'Nipe mwenyewe.'

25. Mtoto aliyezaliwa na mama aliye mtumwa wa watu anakuwa mtumwa wa hao masaidi (mabwana) zake mama yake japokuwa baba yake ni muungwana. Basi wanakatazwa hapa waungwana kuwaoa watumwa wa watu kwani watoto wao watakuwa watumwa.

Lakini akiwa mtu ni masikini, hana uweza wa kuoa mke muungwana — na anajiogopea kuzini—basi atapewa ruhusa kuoa huyo huyo mjakazi; asaa huyo bwana atakapomwona huyo mtoto, atamwonea huruma ampe uungwana. Na ndivyo wanavyohimizwa kufanya hivyo.

Tena wakaliwazwa hao masikini wanaooa wajakazi kuwa mazingatio kwa Mwenyezi Mungu ni dini — si nasaba. Na nyinyi katika dini ni wamoja — nyote Waislamu.

Lakini wanahimizwa waoe wake wazuri wasiozini ovyo ovyo wala kwa kinyumba. Katika zama zao za Ujahili mwanamke aliyekuwa akizini kwa kinyumba (na wanaume makhsusi) hawakuwa wakiona vibaya kumuoa. Wakiona vibaya kumuoa mwanamke aliyekuwa akizini na kila mpita njia. Basi katika Uislamu zinakatazwa zote zina mbili hizo na unaambiwa ujiepushe na kuoa wanawake waliokuwa na feli hizo; ila ikiwa wametubia kweli kweli, unaona kuwa hawataufanya mwendo huo tena.

Na ikatajwa hapa kuwa mjakazi (au mtwana) akizini atiwe nusu ya adabu anayotiwa muungwana. Muungwana anapigwa bakora 100; basi yeye atapigwa 50, kwani muungwana ana vizuwizi vingi vya kumzuia. Nidyo maana kama hakuzuilika atiwe adabu kubwa zaidi.

Na utumwa tumetaja katika Aya ya 177 ya *Suratul Baqarah* kuwa umekatazwa katika Uislamu ila kwa njia moja tu. Wakati wasiokuwa Waislamu wakiwapiga Waislamu, na Waislamu wakapigana nao, wakawa hao wasiokuwa Waislamu wanawafanya mateka Waislamu kuwa watumwa, basi na Waislamu nao watapata ruhusa kuwafanya mateka wa hao kuwa watumwa. Na wakitaka watawaachia bure wende zao kwao au wataachia kwa

أُجُورَهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ مُحْصَنَاتٍ غَيْرَ مُسَافِحَاتٍ
وَلَا مُتَّخِذَاتِ أَخْدَانٍ ۚ فَإِذَا أُحْصِنَّ فَإِنْ أَتَيْنَ
بِفَاحِشَةٍ فَعَلَيْهِنَّ نِصْفُ مَا عَلَى الْمُحْصَنَاتِ مِنَ
الْعَذَابِ ۚ ذَٰلِكَ لِمَنْ خَشِيَ الْعَنَتَ مِنْكُمْ ۚ وَأَنْ
تَصْبِرُوا خَيْرٌ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٢٥﴾

kuzini na kila mtu wala si wenye kuzini na wanaume makhsusi (wa kinyumba). Na wanapoolewa kisha wakafanya ufasiki, basi itakuwa juu yao nusu ya adhabu iliyowekewa wanawake waungwana. Hayo (ya kuoa wajakazi wa watu) ni kwa yule miongoni mwenu anayeogopa kuzini. Na mkisubiri (msiwaoe mpaka mpate fedha za kuoa muungwana) ndio bora kwenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe (na) Mwingi wa Kurehemu.

يُرِيدُ اللَّهُ لِيُبَيِّنَ لَكُمْ وَيَهْدِيَكُمْ سُنَنَ الَّذِينَ
مِنْ قَبْلِكُمْ وَيَتُوبَ عَلَيْكُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٢٦﴾

26. Mwenyezi Mungu anataka kukubainishieni na kukuongozeni katika mwendo wa wale waliokutangulieni, na (anapenda) kukukhafifishieni. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima.

وَاللَّهُ يُرِيدُ أَنْ يَتُوبَ عَلَيْكُمْ وَيُرِيدُ الَّذِينَ
يَتَّبِعُونَ الشَّهَوَاتِ أَنْ تَمِيلُوا مَيْلًا عَظِيمًا ﴿٢٧﴾

27. Na Mwenyezi Mungu anataka kukukhafifishieni. Lakini wanaofuata matamanio (yao) wanataka mkengeuke mkengeuko mkubwa (uliokhalifu haki).

يُرِيدُ اللَّهُ أَنْ يُخَفِّفَ عَنْكُمْ ۚ وَخُلِقَ الْإِنْسَانُ
ضَعِيفًا ﴿٢٨﴾

28. Mwenyezi Mungu anataka kukukhafifishieni maana mwanaadamu ameumbwa dhaifu (hana nguvu kubwa kabisa za kiwiliwili wala nguvu kubwa za kupigana na moyo na shetani).

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ
بِالْبَاطِلِ إِلَّا أَنْ تَكُونَ تِجَارَةً عَنْ تَرَاضٍ مِنْكُمْ ۚ
وَلَا تَقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٢٩﴾

29. Enyi mlioamani! Msiliane mali zenu kwa batili. Isipokuwa iwe biashara kwa kuridhiana baina yenu. (Hiyo inajuzu) wala msijiue (wala msiue wenzenu). Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kukuhurumieni.

وَمَنْ يَفْعَلْ ذَٰلِكَ عُدْوَانًا وَظُلْمًا فَسَوْفَ نُصْلِيهِ
نَارًا ۚ وَكَانَ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿٣٠﴾

30. Na atakayefanya haya kwa uadui na dhulma, basi huyo tutamwingiza Motoni. Na hayo ni rahisi kwa Mwenyezi Mungu.

إِنْ تَجْتَنِبُوا كَبَائِرَ مَا تُنْهَوْنَ عَنْهُ نُكَفِّرْ عَنْكُمْ
سَيِّئَاتِكُمْ وَنُدْخِلْكُمْ مُدْخَلًا كَرِيمًا ﴿٣١﴾

31. Kama mkijiepusha na maovu makubwa mnayokatazwa, tutakufutieni makosa yenu madogo na tutakuingizeni mahali patukufu (kabisa. Napo ni Peponi).

---

vikomboleo. Si lazima kuwafanya watumwa. Yametajwa haya katika Aya ya 4 ya *Surat Muhammad* na huitwa *Suratul Qital.*

29. Hapa inakatazwa kuliana mali kwa njia za batili; inakubalishwa kuuziana kunakopatikana kwa ridhaa ya wote wawili—mwuzaji na mnunuaji. Basi na miamala mingine iliyokubalishwa katika Sharia itakuwa ni kama kuuziana.

Aliposema Mwenyezi Mungu 'Msijiue' imeingia kujiua mwenyewe mtu na kumwua mwenziwe kwani Waislamu wote ni kitu kimoja; na asiyekuwa mwislamu pia huna ruhusa kumuua.

Na katika tamko hili la Kuua inaingia kuua Khasa—akafa mtu mara moja. Na inaingia vile vile kufanya mambo ya kukuhilikisha kidogo kidogo mpaka ukahiliki; kama ulevi na maasi mengine kwani yote hayo yanahilikisha kidogo kidogo. Basi anayeyafanya hayo anaingia katika wanaojiua.

31. Hapa inasemwa kuwa tukijiepusha na ile midhambi mikubwa mikubwa Mungu atatusamehe vile vijidhambi vidogo vidogo, kwani binadamu muhali takriba kusalimika na hivyo vijidhambi vidogo.

Dhambi zote si namna moja. Kuna nyingine mateso yake madogo kwa kuwa dhara yake ni ndogo kwa mkabala wa hizo nyingine. Si kama zile dhambi kubwa kubwa kama:– (a) Kuua (b) Kwiba (c) Kula riba (na kila dhuluma) (d) Kulewa (e) Kuzini (au wanaume kwa wanaume wenyewe). Na kama haya.